MWELEKEO WA SERA ZA CCM KATIKA MIAKA YA 2010 HADI 2020

UTANGULIZI

1. Katika mwaka wa 2000 maamuzi makubwa mawili ya kihistoria yalifanywa nchini Tanzania. Mwanzoni mwa mwaka huo Serikali ilipitisha na kuitangaza Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2000 hadi 2025. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar nayo ikatangaza Dira ya 2000 hadi 2020. Miezi michache baadaye Chama Cha Mapinduzi (Chama Tawala cha wakati huo), kilitangaza Mwelekeo wa Sera za CCM katika Miaka ya 2000 hadi 2010, ukiwa mwongozo wake wa Sera za Kiuchumi na Kijamii za kutekelezwa katika kipindi cha miaka 10 ya kwanza ya Dira 2025 na Dira 2020.

2. Kwa kifupi, Dira ya Maendeleo 2025 ililiwekea Taifa lengo kwamba Watanzania tuchukue hatua za kiuchumi na za kijamii ili ifikapo mwaka 2025 nchi yetu ifikie kiwango cha maendeleo ya kiuchumi ya nchi ya kiwango cha kati. Tanzania kufikia kiwango cha maendeleo ya kati maana yake ni kuwa nchi iliyoondokana na hali ya nchi yenye **uchumi ulio nyuma na tegemezi** na kuwa nchi yenye msingi wa wastani wa uchumi wa kisasa. Maana yake ni kuwa michakato ya mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi, mapinduzi ya viwanda, miundombinu, mawasiliano na ya huduma za kijamii, yawe yamefikia kiwango cha maendeleo cha wastani pia.

3. Chama Cha Mapinduzi, kwa kuelewa kazi kubwa ambayo ingebidi ifanywe na Taifa ili kufikia malengo ya 2025, kilitoa Mwelekeo wa Sera za CCM za 2000-2010 ambao uliainisha **majukumu makuu mawili** ya kutekelezwa kwa msisitizo ambayo ni:-

   (a) Kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea (yaani modenaizesheni ya uchumi) na

   (b) Kutekeleza Sera ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi.

4. CCM iliamini kuwa nguvu za Taifa zikielekezwa kwenye kuyatekeleza majukumu makuu haya kwa njia ya kutekeleza Ilani za 2000 hadi 2005 na ya 2005 hadi 2010, sehemu muhimu ya mwanzo ya reli ya kutufikisha kwenye malengo ya Dira 2025 itakuwa imejengwa. Sura ya Kwanza ya Mwelekeo huu wa sasa ina taarifa na uchambuzi unaoonesha mafanikio makubwa ya maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii yaliyopatikana nchini katika kipindi cha miaka 10 ya utekelezaji wa Mwelekeo huu 2000-2010.

5. Wakati huo huo, mafanikio yaliyopatikana katika nyanja mbalimbali za maendeleo yameibua changamoto nyingi. Hii ni mantiki katika taratibu za maumbile na za jamii. Wajibu wa uongozi ni kuzipatia majawabu changamoto zinazoibuka kutokana na mafanikio ya maendeleo. Mwelekeo wa Sera zetu wa sasa unazishughulikia changamoto zilizoibuka katika kipindi kinachomalizika sasa.

6. Utaratibu wa kujenga nchi kwa kuongozwa na Dira ya Maendeleo unatumika na umetumika na nchi nyingi na hasa nchi changa katika kusukuma maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa ujumla, utaratibu huu umezisaidia nchi nyingi kati ya hizo kupiga hatua za haraka za maendeleo. Nchi zilizofanikiwa, pamoja na mambo mengine, zilitumia utaratibu wa kuwa pia na upangaji wa mipango ya maendeleo kama njia ya kukusanya nguvu za Taifa na kuzielekeza kwenye kufikiwa malengo ya Dira.

7. Chama kina wajibu wa kuupongeza uamuzi wa kimaendeleo uliofanywa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete wa kuunda upya Tume ya Mipango ya Maendeleo. Tume imetenganishwa na Wizara ya Uchumi na Fedha na kuimarishwa ili kushughulikia upangaji maendeleo ulio thabiti kwa kuibua vipaumbele yakinifu, uwiano, mizani na mwelekeo. Uamuzi huu wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete **ni wa kimkakati na umekuja katika wakati muafaka**.

8. Katika **Mwelekeo** huu, msisitizo umewekwa kwenye majukumu makuu mawili yaliyotajwa hapo juu ambayo yakitekelezwa katika miaka kumi ijayo nchi yetu itakuwa imekaribia kufikia malengo ya Dira 2025. Sharti kubwa ni kwamba mpango wa maendeleo utakaoandaliwa kwa kipindi cha 2010-2015 uziweke ahadi zilizomo katika Ilani ya 2010-2015 kwa mujibu wa vipaumbele na uwiano na pia kuhakikisha kuwa kunakuwepo nidhamu katika utekelezaji. Sharti hili litahusu pia utekelezaji wa Ilani 2015-2020.

9. Ni muhimu izingatiwe pia kuwa Zanzibar dira yake ni Dira ya 2020. Inakusudiwa kwamba ifikapo 2020 Zanzibar ifikie maendeleo ya kiuchui ya nchi yenye maendeleo ya kati. Yaani Zanzibar iwe imejenga msingi wa uchumi wa kisasa wa wastani katika fani za viwanda, kilimo, ufugaji, uvuvi, miundombinu, mawasiliano na utalii pamoja na huduma za elimu, afya, maji na nyinginezo kama vile Sekta ya IT.

10. Ili kufikia malengo ya Dira ya Zanzibar ya 2020 lazima majukumu ya jumla ya Mwelekeo huu na yale maalum yatakayokuwemo katika Ilani ihusuyo Zanzibar, nayo yawekwe kwa mpangilio muafaka katika mpango wa maendeleo wa Zanzibar wa 2010-2015 na wa 2015-2020. Kwa kuwa dira ya Zanzibar ni 2020, sasa tumebakiwa na miaka 10 tu kuyafikia malengo yake. Maana yake ni kuwa mbele yetu tuna Ilani mbili tu za kutekelezwa

ili kufikia malengo tuliyojiwekea katika Dira ya Zanzibar ya 2020. Utaratibu wa kuwa na Tume ya Mipango ukitumika ndio utakaotuhakikishia kufikia malengo hayo kwa uhakika.

11. Sisi wenyewe ndio tulioamua kuwa tujiwekee Dira ya Maendeleo ya nchi yetu. Serikali ya Muungano wa Tanzania ikajiwekea Dira 2025 na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ikajiwekea Dira 2020. Kazi ambayo tumeifanya kwa miaka kumi inayomalizika sasa ni nzuri. Lakini kazi ya kufanya iliyo mbele yetu hadi 2020 kwa Zanzibar na 2025 kwa Jamhuri ya Muungano ni ngumu zaidi na kubwa zaidi. Lakini changamoto hii tunaiweza na lazima tuiweze.

12. Katika historia yetu, Chama kimefanikiwa kuongoza mambo makubwa ya maendeleo ya kupigiwa mfano. Baadhi ya hayo ni yafuatayo:-

    (a) Chini ya uongozi wa Baba wa Taifa Mwl. J.K. Nyerere:-

        (i) Iliwezekana kufuta ujinga wa kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa asilimia zaidi ya 95 (tukawa wa pili katika dunia kufanya hivyo baada ya Cuba).

        (ii) Iliwezekana kutekeleza UPE (Azimio la Musoma) kati ya 1977 hadi miaka ya themanini na kufanikiwa kwa zaidi ya 90%.

        (iii) Iliwezekana kuyachapa na kuyashinda majeshi ya uvamizi ya Nduli Iddi Amin Dada 1978-1979.

    (b) Utekelezaji wa UPE uliposuasua katika miaka ya 80 na 90, Rais Mstaafu Benjamin Wiliam Mkapa wa Awamu ya Tatu iliongoza nchi katika kuhuisha UPE kwa mpango wa MMEM ili mafanikio ya kurudi kwenye kiwango cha zaidi ya 95%.

    (c) Chini ya uongozi wa Rais Jakaya Marisho Kikwete wa Awamu hii ya Nne katika miaka mitano yake ya kwanza mambo makubwa kadhaa yamefanyika. Hapa chini ni mifano mitatu:-

        (i) Imewezekana kujenga shule za sekondari katika kila Kata ambapo tangu 2005 hadi sasa 2010, idadi ya shule za sekondari nchini imeongezeka kutoka 1,745 mwaka 2005 hadi 4,102 na wanafunzi walioko kidato cha kwanza mpaka cha nne wameongezeka kutoka 401,598 mwaka 2005 hadi 1,401,559 mwaka 2010.

        (ii) Wanafunzi wa vyuo vikuu wameongezeka kutoka 55,296

mwaka 2005 hadi 82,428 mwaka 2010.

(iii) Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kutokana **na ubunifu na dhamira yake ya kisiasa** ya kusukuma maendeleo ya elimu kwa kasi zaidi, imewezekana kuanzisha na kukijenga Chuo Kikuu cha Dodoma chenye lengo la kufikia wanafunzi 40,000 kitakapokamilika ambapo katika mwaka wake huu wa nne tayari kina wanafunzi wapatao 19,000. Watanzania na wageni wanaopata fursa ya kuvinjari Chuo Kikuu cha Dodoma wanaondoka wakikiri kuwa umahiri wa uongozi na utaalam unajidhihirisha katika kazi ya kuibua chuo hiki na ukubwa wa wazo lenyewe lililoanzisha mchakato wa ujenzi wa chuo hiki hutokea kwa nadra sana katika nchi zetu changa.

13. Tumeorodhesha mifano hii ili kuonesha kuwa Watanzania tuna uwezo mkubwa wa kufanikisha mambo mazito yenye maslahi kwa nchi yetu na watu wake. Hivyo tunao uwezo wa kupambana mpaka kufikia malengo ya Dira 2020 kwa Zanzibar na Dira 2025 kwa Tanzania Bara. Utekelezaji wa Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000 hadi 2010 na Ilani zake mbili za miaka mitano mitano ijayo ndiyo njia ya uhakika ya kufikia malengo hayo ya Dira.

14. Pamoja na sera na mikakati mizuri, tutafanikiwa kufikia malengo ya Dira 2020 kwa Zanzibar na ya Dira 2025 kwa Tanzania Bara tukidhamiria kuzingatia masharti yaliyozisaidia nchi nyingine zinazoendelea kujiondoa kwenye hali dhalili ya uchumi ulionyuma na tegemezi na kufikia zilipo sasa nchi zenye uchumi wa maendeleo ya kati. Baadhi ya mambo ya kuzingatia ni haya yafuatayo:-

(a) Viongozi kuwa na **uelewa unaofanana** kuhusu maana ya **majukumu makuu** ya Mwelekeo wa CCM katika kipindi cha miaka kumi ijayo. Ni muhimu tuelewane juu ya maana ya kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linaojitegemea. Lakini tuelewane kwanza juu ya dhana ya uchumi ulio nyuma na tegemezi. Tukiielewa maana ya uchumi ulionyuma na tegemezi ndipo tutakapoielewa vizuri kazi iliyo mbele yetu ya kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea. Tuelewane pia juu ya Sera ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, tubaini umuhimu wa sera hii na ujenzi wa uchumi wetu n.k.

Uelewa mmoja wa sera unajenga mshikamano katika fikra na kuondoa mkanganyiko katika kutoa ujumbe kwa watendaji kwa jamii. Kutokana na umuhimu wa hoja hii, CCM ikishinda katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 na kuunda Serikali, itazitaka Serikali zihakikishe kuwa kunaendeshwa semina za viongozi na watendaji wakuu katika ngazi za taifa, mikoa, wilaya hadi kata na vijiji kwa lengo la kujenga uelewa mmoja juu ya majukumu yaliyo mbele yetu. Hii ni methodolojia muhimu kuelekea kufanikisha utekelezaji wa majukumu.

(b) **Nchi yetu kurudisha utaratibu wa kuwa na mipango ya maendeleo ya miaka mitano mitano**. Awali tumepongeza uamuzi wa Serikali ya Awamu ya Nne wa kuunda upya Tume ya Mipango. Hatua zichukuliwe sasa za kuandaa Mpango wa Maendeleo wa 2010-2015 kwa msingi wa Ilani ya Chama kitakachoshinda katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010.

Utekelezaji wa Mwelekeo wa CCM 2010-2020 na wa Ilani zake za 2010-2015 na 2015 -2020 utapata msukumo maalum kutokana na kuundwa upya kwa Tume ya Mipango na kuanzishwa kwa utaratibu wa kuwa na mipango ya maendeleo ya miaka mitano mitano. Tume ya Mipango ina umuhimu wa pekee kwa sababu itafanya kazi za:-

(i) Kuwa kituo cha chemchem ya fikra (think tank) cha Taifa kuhusu maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

(ii) Kuainisha vipaumbele vya maendeleo ya nchi kulingana na hali halisi.

(iii) Kuwa chombo cha kupanga na kugawa rasilimali watu na rasilimali fedha kwa hekima na usahihi.

(iv) Kuwa chombo cha kuweka uwiano katika mchakato wa maendeleo ya nchi.

(v) Kuwa chombo cha kuweka nidhamu katika mpangilio wa shughuli zilizopangwa na utekelezaji wake.

(vi) Kuwa chombo cha kuratibu uchumi na kutathmini utekelezaji wa mpango.

(c) Nchi za Asia zilizopata maendeleo ya haraka hazikuwa na umaarufu katika nyanja za demokrasia na utawala bora. Sisi tumeamua kuwa na mfumo wa demokrasia na utawala bora kwa hiari yetu na ni lazima tuendelee hivyo kwani uhuru na heshima ni lengo na pia ni kichocheo cha maendeleo ya binadamu.

Lakini Watanzania tunajua kuwa katika mambo makubwa ya kupigiwa mfano ambayo tumeyafanikisha kama taifa nyenzo kubwa iliyotufanya tufanikiwe ni **dhamira ya kisiasa ya uongozi wa juu kabisa wa nchi yetu**. Wote tunaikumbuka kauli maarufu ya Baba wa Taifa, Mwl. J.K. Nyerere "**Tuna kazi moja tu, ni kumpiga! Sababu tunazo. Uwezo tunao. Na nia tunayo".** Na vijana wa Tanzania, wapiganaji wa Tanzania, wakampiga Nduli Iddi Amini Dada mpaka akaikimbia nchi yake.

Na katika mifano mingine michache iliyotajwa hapo juu, uongozi wa juu kabisa wa nchi ulikuwa na **dhamira ya kisiasa** na dhamira hiyo ikaenea kwa viongozi wengine, watendaji na kwa wananchi kwa ujumla. Ndiyo maana tukafanikiwa. Kazi iliyo mbele yetu itahitaji viongozi wenye dhamira ya kisiasa na nidhamu inayoendana nayo. Hivyo, tunahitaji viongozi wenye kuweka mbele maslahi ya nchi na siyo maslahi binafsi.

(d) Sharti la nne la kutuletea mafanikio katika harakati zetu kuelekea malengo ya Dira 2020 na Dira 2025 ni kutekeleza sera ya diplomasia ya uchumi katika maana pana. Tangu Rais Jakaya Mrisho Kikwete aingie madarakani amefanikiwa kujenga mahusiano mazuri na makubwa na mataifa na taasisi za kimataifa mbalimbali kama alivyofanya mtangulizi wake Rais Mstaafu Benjamin Mkapa. Matokeo yake ni kuwa nchi yetu imefanikiwa kiuchumi na kijamii. Chama chetu kitapenda diplomasia hii ya kiuchumi iendelezwe.

Changamoto inayojitokeza ni kuwa baadhi ya watendaji wetu wakuu wa Serikali wenye nafasi ya kimkakati katika kufanya diplomasia ya kiuchumi ili kuvutia wawekezaji wa aina mbalimbali hawajitumi vya kutosha. Tabia ya kuchelewa kuamua, kuwazungusha wawekezaji wa nje na wa ndani badala ya

kuwaharakishia mahitaji yao zinasambaa na zimeota mizizi. Taarifa za hivi sasa zinasema kuwa mwekezaji ajaye Tanzania anangoja kwa muda mrefu zaidi ili kupata majibu ya kuwekeza nchini kuliko wawekezaji waendao nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Chama Cha Mapinduzi kitazitaka Serikali kulifanya suala la utekelezaji wa diplomasia ya kiuchumi linatelekezwa kwa umakini na umahiri Serikalini kote. Ili kufanikisha utekelezaji wa Ilani kuelekea malengo ya Dira zetu tutaendelea kuhitaji uwekezaji, mikopo na sayansi na teknolojia za kisasa kutoka nje.

SURA YA KWANZA

TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MWELEKEO WA SERA ZA CCM KATIKA MIAKA YA 2000 HADI 2010

15. Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama Cha Mapinduzi uliofanyika mjini Dodoma, tarehe 10 Juni 2000, ulipitisha na kutangaza Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000 hadi 2010. Mwelekeo huo ndio ulikuwa dira ya kukiongoza Chama chenyewe na Serikali zake katika kuainisha majukumu, kupanga malengo na mikakati ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya nchi yetu.

16. Mwelekeo huo ulibainisha kinagaubaga kuwa uchumi wetu unazo sifa kuu mbili: Uchumi ulio nyuma na ni tegemezi. Kutokana na ukweli huo Malengo makuu katika kipindi hicho yaliendelea kuwa:-

    (a) **Kujenga Msingi wa Uchumi wa Kisasa wa Taifa linalojitegemea unaosukumwa na Sayansi na Teknolojia**.

    (b) **Kujenga mazingira ya uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi**.

17. Malengo haya mawili ni muendelezo wa Malengo makuu ya Mwelekeo wa sera za CCM katika miaka ya Tisini, ambao kwanza ulitamka kuwa siasa ya msingi ya CCM itaendelea kuwa ni Ujamaa na Kujitegemea ambayo, ndio iliyotujengea mazingira ya amani, utulivu na umoja wa Taifa letu na inayoendana na matarajio ya wananchi waliowengi. Aidha, Mwelekeo huo ulisisitiza kuwa, lengo la Ujamaa na Kujitegemea ni kuhakikisha kwamba uchumi wa Tanzania unamilikiwa na kuendeshwa na wananchi wenyewe kwa njia mbalimbali. Hii ni sera ambayo utekelezaji wake ni wa muda mrefu na inahitaji mipango na mikakati thabiti.

18. **Pili**, Mwelekeo huo ulibainisha kwamba, lazima nguvu na uwezo wetu uelekezwe kwenye kuinua kiwango cha nguvu za uzalishaji mali ili kuinua uchumi wa Taifa. Kwa sasa unatumia kiwango kidogo cha maarifa katika uzalishaji, vitendea kazi duni na miundombinu ya uzalishaji mali iko nyuma. Hivyo, kazi iliyo mbele yetu ni **kuwajenga wananchi kwa elimu na maarifa ya kisasa na kujenga miundombinu ya kisasa**.

19. Tathmini ya utekelezaji wa Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000 hadi 2010, imegawika katika vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Malengo ya kila kipindi yameainishwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000-2005 na ya mwaka 2005-2010. Ilani hizo zote ziliandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Mwelekeo huo.

20. Kipindi cha kwanza cha utekelezaji wa Mwelekeo wa Sera za CCM katika

miaka ya 2000 hadi 2010 kilitekelezwa sambamba na kipindi cha pili na cha mwisho cha Serikali ya Awamu ya Tatu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya uongozi wa Rais Mstaafu Mhe. Benjamin William Mkapa. Kipindi cha pili na cha mwisho cha utekelezaji wa Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000-2010 kilitekelezwa katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya uongozi wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kufuatia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

21. Katika kipindi hiki, Serikali imeweza kutekeleza kwa mafanikio makubwa Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000-2010. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wake iliandaa Dira ya Maendeleo ya 2025 paoja na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA) ili kutekeleza Malengo ya Milenia. Aidha, Serikali ilitoa kipaumbele katika masuala yafuatayo:-

    (a) Kutekeleza Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, ili kuiondolea Serikali mzigo wa kuendesha uchumi moja kwa moja. Lengo la sera hii ni kujenga mazingira ya kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji wa bidhaa za viwandani na kuiwezesha Serikali kukusanya kodi, badala ya kuendelea kutoa ruzuku kwa mashirika yake.

    (b) Kujenga mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji, na kupitishwa Sera na Sheria ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, kupambana na rushwa na kuziba mianya ya ukwepaji wa kulipa kodi.

    (c) Kutekeleza Sera ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, kwa kuwapatia fursa za mikopo ili kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kupambana na umasikini.

    (d) Kupitishwa sheria kadhaa zikiwemo za mikopo na karadha "Lease Financing), mikopo ya nyumba (Mortgage finance)" na umilikishaji sehemu ya nyumba (Unit title or Condominium) ambazo ni nyenzo na fursa muhimu za kuwawezesha wananchi kiuchumi.

22. Hatua hii ya Serikali iliwezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kama ifuatavyo:-

Uchumi

(a) Uchumi umeendelea kuimarika na kukua kwa wastani wa asilimia 6.7 kwa mwaka.

(b) Mfumko wa bei ulibaki katika tarakimu moja, tangu mwaka 2000 hadi 2007 isipokuwa mwaka 2008 ulifikia kiwango cha asilimia 10.3 kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani.

(c) Wastani wa pato la kila Mtanzania kwa mwaka liliongezeka kutoka TShs. 255,573 mwaka 2000 hadi TShs. 629,884 mwaka 2008.

(d) Bajeti ya sekta ya kilimo imeongezeka kutoka asilimia 4.7 mwaka 1999/2000 hadi asilimia 7.9 mwaka 2009/2010.

(e) Mauzo nje yameongezeka kutoka trilioni 1.9 mwaka 2005 hadi trilioni 3.7 mwaka 2009.

(f) Tanzania ilitimiza masharti ya **Mpango wa Msamaha kwa Nchi Masikini Zenye Madeni Makubwa** mwezi Novemba, 2001. Fedha ambazo zingetumika kulipia madeni yaliyofutwa zilielekezwa katika sekta teule za huduma za kijamii, kiuchumi na miundombinu ambazo zinawagusa wananchi moja kwa moja.

Miundombinu

23. Katika kipindi hiki Serikali imeongeza bajeti ya sekta ya Miundombinu kutoka Tsh. bilioni 344.8 mwaka 2005 hadi Tsh. 801.0 bilioni mwaka 2009. Hatua hii imewezesha kukua na kuimarika kwa huduma ya barabara, reli, viwanja vya ndege na bandari.

Barabara za Vijiji na Halmashauri

24. Katika uchaguzi wa 2005, CCM iliahidi kuongeza fedha katika Mfuko wa Barabara ili kuziongezea fedha Halmashauri za Wilaya za kuimarisha muundombinu huu muhimu kwa maendeleo. Ahadi hiyo tumeitimiza. Hivi sasa bajeti ya barabara kwa Halmashauri za Wilaya ni Tsh. bilioni 65 kutoka Tsh. bilioni 21.5 mwaka 2005. Hili ni ongezeko la mara tatu. Kwa sababu hiyo barabara nyingi zimefanyiwa matengenezo na mpya kujengwa.

25. Kwa upande wa barabara za vijijini kilometa 1,407 za barabara, madaraja 71, makalavati 1,056 na drifti 79 yametengenezwa. Kwa upande wa barabara za wilaya, barabara zenye hali nzuri zimeongezeka kutoka kilomita 600 mwaka 2005 hadi kilomita 1500 mwaka 2008 sawa na

ongezeko la kilomita 900.

Barabara za Mikoa

26. Katika kipindi hiki mtandao wa barabara za mikoa umeongezeka kutoka urefu wa kilometa 10,957.4 hadi kilometa 19,246, mwaka 2009. Kati yake kilometa 635 ni za lami na kilometa 18,611 ni za changarawe.

Barabara Kuu

27. Mtandao wa barabara kuu umeongezeka na kufikia kilometa 10,601. Kati ya hizo kilometa 5,065.4 ni za lami na kilometa 5,307.7 ni za changarawe ndogo.

Mawasiliano

28. Kumekuwa na maendeleo makubwa ya mawasiliano ya simu, hususan simu za mkononi kuliko la simu za mezani. Hadi Mei 2010 Watanzania wenye simu ni 18,381,390 na kati ya hao wenye simu za mkononi 18,207,390. Kwa nia ya kuendeleza mawasiliano Serikali imeanza ujenzi wa mkongo wa Taifa ambao umekwishafika hadi mipakani mwa nchi jirani za Ruanda, Uganda, Burundi na Kenya. Mkongo huo sasa unaelekea Tunduma mpakani mwa Zambia. Utakapokamilika gharama za simu na intaneti zinatarajiwa kushuka kwa kiwango kikubwa.

29. Kwa upande wa habari na utangazaji Serikali ya CCM imeendelea kudumisha uhuru wa vyombo vya habari nchini. Matokeo ni kuwepo kwa magazeti 108, radio 68 na Televisheni 27.

HUDUMA ZA JAMII

Elimu

30. Kwa kushirikiana na wananchi na kwa kupitia programu na miradi mbalimbali kama vile MMEM, MMES na MEMKWA mafanikio makubwa yamefikiwa kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari, ufundi hadi elimu ya juu. Elimu ya watu wazima na elimu maalumu nayo imepewa msukumo maalumu.

Elimu ya Awali

31. Idadi ya wanafunzi wa Elimu ya awali imeongezeka kutoka 638,591 mwaka 2005 hadi 873,981 mwaka 2008, wakiwemo wanafunzi 2,146 wenye mahitaji maalumu.

Elimu ya Msingi

32. Idadi ya wanafunzi wa shule za msingi imeongezeka kutoka 7,541,208 mwaka 2005 na kufikia 8,410,208 mwaka 2008 wakiwemo wanafunzi 34,661 wenye mahitaji maalumu. Shule za msingi zimeongezeka kutoka 14,257 mwaka 2005 na kufikia 15,673 mwaka 2008.

Elimu ya Sekondari

33. Idadi ya wanafunzi wa Sekondari wanafunzi waliojiunga na kidato cha kwanza wameongezeka kutoka 180,239 mwaka 2005 na kufikia 524,784 mwaka 2009. Idadi hii inafanya wanafunzi wa sekondari kidato cha 1 hadi 6 kuongezeka kutoka 524,325 mwaka 2005 na kufikia 1,466,402 mwaka 2009. Shule za sekondari ziliongezeka kutoka 1,745 mwaka 2005 na kufikia 4,102 mwaka 2009.

Vyuo vya Ufundi

34. Udahili wa wanafunzi wa vyuo vya ufundi umeongezeka kutoka 40,059 mwaka 2005/2006 hadi kufikia 48,441 mwaka 2007/2008. Ongezeko hili limechangiwa na kuongezeka kwa vyuo vya ufundi kuwa 210 mwaka 2008 kutoka 183 mwaka 2005. Pia vyuo vya ufundi stadi vimeongezeka kutoka 260 mwaka 2005 hadi 932 mwaka 2009.

Elimu ya Juu

35. Wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu vilivyopo nchini waliongezeka kutoka 55,296 mwaka 2005/2006 hadi 82,428 mwaka 2007/2008. Kati yao wanafunzi 69,000 walipata mikopo ya elimu ya juu, ambapo jumla ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya mikopo iliongezeka kutoka Tshs. 56.1 bilioni mwaka 2005/2006 hadi Tshs. 117 bilioni mwaka 2007/2008.

36. Katika kuendeleza elimu ya awali, msingi na sekondari kuna changamoto kubwa nne.

    (a) Upungufu wa walimu.
    (b) Upungufu wa vitabu na vifaa vya kufundishia
    (c) Upungufu wa maabara kwa shule za sekondari.
    (d) Upungufu wa nyumba za walimu.

Serikali imekuwa inachukua hatua mbalimbali kupunguza na hatimaye kumaliza matatizo hayo.

Mafunzo ya Ualimu

37. Ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeendeleza mafunzo ya ualimu na kuweza kuongeza idadi ya walimu wa awali, msingi na sekondari, vyuo vya ualimu, vyuo vya ufundi na vyuo vikuu. Hadi kufikia mwaka 2008 vyuo 79 nchini vimekuwa vikitoa mafunzo ya ualimu. Kati ya vyuo hivyo 34 ni vya Serikali na 45 ni vya watu na mashirika binafsi. Idadi ya vyuo vikuu imeongezeka kutoka 26 mwaka 2005 hadi kufikia 32 mwaka 2008. Kati ya hivyo vipya kimoja ni cha Serikali kinachojengwa Dodoma ambacho kitakapokamilika kitakuwa na wanafunzi 40,000 na kuwa ndicho kikubwa kuliko vyote nchini.

38. Hatua hizi za Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi zimesaidia kuongeza idadi ya walimu na kupunguza upungufu. Idadi ya walimu wa awali iliongezeka kutoka 11,148 mwaka 2005 na kuwa 16,597 mwaka 2008. Walimu wa shule za msingi waliongezeka kutoka 135,013 mwaka 2005 na kufikia 154,895. Idadi ya walimu wapya wa sekondari wanaohitimu katika vyuo vikuu hapa nchini imeongezeka kutoka 500 mwaka 2005 hadi 2,843 mwaka 2008 na mwaka huu 2010 wamefikia 5,331. Walimu wa elimu maalumu wameongezeka kutoka 1,522 hadi 1,972.

39. Kuhusu vitabu na vifaa vya kufundishia, nyongeza kubwa iliyofanyika katika bajeti ya sekta ya elimu ilikuwa na maana ya kujenga uwezo wa kukabiliana na tatizo hilo. Bajeti ambayo ni karibu Tsh. trilioni 1.4 ndiyo kubwa kuliko zote. Aidha, wabia wetu wa maendeleo nao wamejitokeza kutusaidia katika jambo hili muhimu. Serikali ya Marekani imejitolea kutuchapishia vitabu vya hesabu na masomo ya sayansi. Benki ya Maendeleo ya Afrika itatupatia mkopo wa kujenga maabara na kununulia vifaa vya maabara. Misaada hiyo ikijumuishwa na jitihada zetu itatusogeza sana mbele katika kuwapatia watoto wengi elimu iliyo bora.

40. Kwa upande wa upungufu wa nyumba za walimu Serikali imeongeza fedha za ujenzi wa nyumba za walimu nchini kote.

Afya

41. Utoaji wa huduma za Afya uliendelea kuboreshwa kwa kiasi kikubwa. Kutoka mwaka 2005 hadi 2008, jumla ya zahanati 464, vituo vya afya 98 na nyumba za waganga 394 zilijengwa. Aidha, zahanati 1,037, vituo vya afya 285 na hospitali 112 zimekarabatiwa. Hali hii inafanya zahanati ziongezeke na kuwa 6,462 katika mwaka 2008 kulinganisha na zahanati 5,323 mwaka 2006. Vituo vya afya vimeongezeka kutoka 526 hadi kufikia 663 mwaka 2008. Aidha, katika kuleta ufanisi wa huduma za afya, mashine za kuchunguza damu, uwezo wa figo na ini pamoja na mashine za X-ray zimewekwa katika kila hospitali ya wilaya na huduma za maabara zimeimarishwa.

Maji

42. Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita Serikali imeendeleza juhudi za kuwapatia wananchi wa Tanzania maji safi na salama. Mpaka mwaka 2008 kwa vijijini upatikanaji wa maji ulifikia asilimia 58.3 na mijini asilimia 80.3. Miradi 138 imekamilika katika wilaya mbalimbali hapa nchini na wananchi wanapata maji safi na salama.

43. Miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi hiki ni kukamilika kwa mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria. Mradi huu wa aina yake na wa kihistoria unawahakikishia wananchi wapato milioni moja katika Mikoa ya Shinyanga na Mwanza kupata maji safi na salama.

44. Katika kipindi hiki Serikali imeendelea kufanya kazi ya kuifanyia matengenezo miradi ya maji iliyopo ili watu waendelee kupatiwa huduma ya maji safi na salama. Jumla ya miradi 53 ya maji katika miji mikuu ya wilaya na miji midogo imefanyiwa ukarabati. Aidha, miradi 7 ya Taifa na 8 ya miji mikuu ya wilaya imekarabatiwa.

Utekelezaji wa Mwelekeo wa Sera za CCM katika Miaka ya 2000-2010 kwa upande wa Zanzibar.

45. Kwa upande wa Zanzibar, utekelezaji wa Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000 hadi 2010, umesadifu kwenda sambamba na kipindi cha miaka kumi ya Awamu ya Sita ya Serikali ya Mpinduzi Zanzibar (2000-2010). Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2000-2005 na ile ya mwaka 2005-2010, zilitekelezwa na Awamu ya Sita ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, chini ya uongozi wa Rais Amani Abeid Karume.

46. Serikali (SMZ) iliandaa Dira ya Zanzibar ya 2020, Mpango wa Kupunguza Umasikini–Zanzibar (ZPRP), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA) na kufanya jitihada za makusudi kurejesha imani ya Washirika wa Maendeleo ili kuunga mkono jitihada za Wananchi wa Zanzibar na Serikali yao katika kujiletea maendeleo. Jitihada za kuimarisha demokrasia, usimamizi bora wa uchumi, amani na utulivu wa kisiasa ni mambo yaliyoimarisha mashirikiano na Washirika wa Maendeleo.

47. Ili kuimarisha uchumi, Serikali (SMZ) ilifanya mageuzi makubwa ya kiuchumi na kutekeleza hatua zifuatazo:-

(a) Kufanya mapitio ya sheria ya kodi na Makampuni na kuimarisha udhibiti wa mapato na matumizi ya Serikali.

(b) Kufungua hesabu zake katika Benki Kuu (BOT) na kuanzisha mfumo wa "Central Payroll Unit" pamoja na kuimarisha usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa kuanzisha mtandao wa kompyuta kwa ajili ya kazi hiyo (Intergrated Financial Management System).

(c) Sera mpya ya Uwekezaji na Sheria ya kulinda na kuhifadhi vitega uchumi ambayo ina vivutio vingi zaidi kwa wawekezaji zimekamilika na kuunda Mamlaka moja ya Uwekezaji. Uanzishwaji wa Sera na Sheria hizi umeongeza kasi ya uingiaji wa fedha za nje kutoka thamani ya T.Sh. 37.8 bilioni mwaka 2000 hadi T.Sh. 175.9 bilioni mwaka 2009. Kiwango hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 32.2 kwa mwaka, na uwiano wa uwekezaji kwa pato la Taifa umepanda kutoka asillimia 12.8 mwaka 2000 hadi asilimia 20.1 mwaka 2009.

(d) Sheria ya Mitaji ya Umma ya mwaka 2002, imepitishwa ili kuyawezesha Mashirika ya Serikali kujiendesha kibiashara.

(e) Shirika la Uvuvi na Mashamba ya Mipira yamefanyiwa tathmini na kukodishwa; Kiwanda cha Maziwa kimefanyiwa tathmini na kuuzwa kwa Mwekezaji wa ndani.

48. Kutokana na jitihada hizi za Serikali, mafanikio yafuatayo yaliweza kupatikana:-

i) Ukuaji wa pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 4.9 mwaka 2000 na kufikia wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2009.

ii) Kasi ya mfumko wa bei imeendelea kushuka kutoka asilimia 18.5 mwaka 2004 na kufikia asilimia 8.9 mwaka 2009.

(iii) Pato kwa kila mwananchi limeongezeka kutoka kiwango cha Tshs. 325,000 (US$ 248) mwaka 2004 na kufikia Tshs. 726,000 (US$ 555) mwishoni mwa mwaka 2009.

(iv) Kiwango cha ukusanyaji wa mapato ya ndani yanayosimamiwa na Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) umeongezeka kutoka T.Shs. 17.15 bilioni mwaka 2000/2001 hadi T.Shs. 103.95 bilioni mwaka 2008/2009.

49. Aidha, mafanikio haya ya kiuchumi yaliiwezesha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kutekeleza miradi mbambali ya maendeleo na kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na huduma za kijamii na kupata mafanikio yafuatayo:-

(a) Kutekeleza miradi ya jamii inayohusu elimu, afya, kilimo, mifugo, uvuvi na utunzaji wa mazingira (TASAF, ASSP/ASDP-L, PADEP na MACEMP).

(d) Kufufua kituo cha kuzalisha mbegu bora za nafaka Bambi.

(c) Kuendeleza ujenzi wa barabara za lami mijini na vijijini.

(d) Kukamilisha ujenzi wa bandari ya Malindi pamoja na sehemu ya kuteremkia abiria.

(e) Kukamilisha ujenzi wa jengo la kupumzikia abiria, uzio wa kuzungushia eneo la bandari na ukuta wa kuzuia mmonyoko wa ardhi katika eneo la bandari ya Mkoani Pemba na kuitangaza kuwa mlango mkuu wa kuingilia nchini.

(f) Kukifanyia matengenezo makubwa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Zanzibar na kuweza kuhudumia ndege kubwa. Aidha, kiwanja cha ndege cha Karume-Pemba, kimefanyiwa matengezo na kupatiwa gari la zimamoto.

(g) Kuendeleza kazi ya usambazaji umeme mijini na vijijini, Unguja na Pemba. Aidha,kisiwa cha Pemba ambacho kwa muda mrefu kilitumia umeme wa "Generator", kimeweza kuunganishwa na Gridi ya Taifa na kupata umeme wa uhakika kutoka Tanga na kufanya visiwa vyote vya Zanzibar kuwa na umeme wa uhakika wa gridi.

(h) Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) kimeanzishwa na ujenzi wa jengo jipya la Chuo hicho huko Tunguu mkoa wa Kusini Unguja umeanza.

(i) Kuimarisha Hospitali kuu ya Mnazi Mmoja kwa kufanya ukarabati wa sehemu zote muhimu na kuipatia vifaa vya kisasa. Aidha,huduma ya Matibabu ya Haraka(Fast Track) imeanzishwa.

(j) Kujenga jengo jipya la huduma kwa waathirika wa UKIMWI VCT (Gold Standard) pamoja na Maabara mpya ya damu salama .

(k) Hospitali ya Chake Chake imepatiwa mashine za kuchunguza VVU, ECG pamoja na vifaa vya upasuaji. Hospitali ya Wete nayo imepatiwa "Solar Power" pamoja na sehemu ya kuhifadhia damu.

(m) Kupambana na ugonjwa wa malaria kwa kufukiza dawa ya mbu majumbani, sambamba na ugawaji wa vyandarua vyenye dawa kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.Hatua hii imeiwezesha Zanzibar kuudhibiti ugonjwa huo kwa kiwango cha asilimia 98.

(n) Kuendeleza kazi ya usambazaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa mijini kutoka kiwango cha asilimia 70 mwaka 2000 hadi asilimia 80 mwaka 2010 kwa maeneo ya mijini na kutoka asilimia 41 mwaka 2000 hadi asilimia 60 mwaka 2010 kwa maeneo ya vijijini.

(o) Kuanza mchakato wa maandalizi ya mradi wa ujenzi wa njia ya pili ya umeme inayopita chini ya bahari kutoka Ras-Kiromoni Tanzania Bara hadi Fumba (mradi wa MCC).

Usawa wa Jinsia

50. Kwa kuzingatia imani ya CCM juu ya usawa wa binadamu na wito wa kimataifa juu ya usawa wa jinsia, Serikali chini ya uongozi wa CCM imeweza kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi mbalimbali za uongozi na utendaji Serikalini na katika Taasisi za Umma.

(b) Kuanzisha Benki ya Wanawake.

(c) Kupitisha Sheria ya Mtoto.

Changamoto zilizojitokeza.

51. Maendeleo ya kweli ni mchakato endelevu. Kwa kuzingatia ukweli huu ni wazi kuwa, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka kumi ya utekelezaji wa Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000 hadi 2010, zipo pia changamoto kadhaa zilizojitokeza katika kipindi hicho. Baadhi ya changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

    (a) Haja ya kuwa na mpango kabambe wa kuandaa watalamu wanaotakiwa katika huduma za uchumi na jamii kwa kuzingatia kukua kwa uchumi na ongezeko la watu nchini.

    (b) Haja ya kuongeza watalamu katika sekta za huduma za jamii hususan sekta ya elimu na afya.

    (c) Haja ya kukuza matumizi ya Sayansi na Teknolojia katika shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi miongoni mwa wananchi na Taifa kwa jumla.

    (d) Haja ya kujenga nyumba za kutosha za walimu na watumishi wa afya, maabara za shule, vituo vya afya na kuwapatia vitendea kazi.

    (e) Ukosefu wa mitaji kwa wajasiriamali kutokana na kuwepo kwa masharti magumu ya mikopo kutoka vyombo vya fedha.

    (f) Uhaba wa nishati ya umeme na miundombinu duni ya kiuchumi, hali ambayo huathiri kiwango cha uzalishaji wa bidhaa, huduma bora na tija.

    (g) Urasimu mkubwa katika uanzishaji wa miradi ya kiuchumi kwa wawekezaji pamoja na gharama kubwa za uendeshaji wa biashara, ikilinganishwa na nchi nyingine.

    (h) Usimamizi usioridhisha wa fedha za umma katika Halmashauri za Wilaya.

    (i) Udhaifu wa uongozi na ubadhirifu wa mali na fedha kwa vyama vya ushirika.

52. Hivyo basi, mafanikio ya Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000 hadi 2010 pamoja na changamoto zake yanaendelea kuwa jukwaa linalotuunganisha na majukumu ya Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2010 hadi 2020.

SURA YA PILI

UJENZI WA MSINGI WA UCHUMI WA KISASA WA TAIFA LINALOJITEGEMEA

53. Kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana kutokana na utekelezaji wa Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000 hadi 2010 na changamoto zake, malengo makuu ya Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2010 hadi 2020 yatakuwa yafuatayo:-

(a) Kupambana kikamilifu na suala la uchumi duni na tegemezi kwa kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea unaozingatia matumizi ya kiwango cha juu cha maarifa yatokanayo na sayansi na teknolojia;

(b) Kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwapa elimu ya kisasa itakayowawezesha kufanikisha Mapinduzi katika kilimo na ujasiriamali;

(c) Kutumia kikamilifu fursa ya kijiografia ya nchi yetu katika kujenga na kuimarisha uchumi na kuifanya Tanzania kuwa Lango Kuu la biashara ya kuingia na kutoka katika kanda ya Afrika Mashariki na Kati;

(d) Kurejesha mfumo wa Upangaji wa Mipango na usimamizi wa uchumi ili kuipa Dola nafasi ya kuwa mhimili wa uchumi katika mazingira ya ujenzi wa msingi wa uchumi wa kisasa wa Ujamaa na Kujitegemea katika mazingira ya uchumi wa soko na utandawazi;

(e) Kuwa na Mpango kabambe wa kuendeleza rasilimali watu unaozingatia mahitaji na ugavi halisi wa taaluma mbali mbali katika maendeleo ya nchi yetu.

(f) Kujizatiti ili tuwe washindani mahiri katika soko la pamoja la Afrika Mashariki.

Mkakati wa Kujenga Msingi wa Uchumi wa Kisasa wa Taifa Linalojitegemea (Modenaizesheni)

54. Kazi ya kujenga msingi wa kisasa wa uchumi wa Taifa linalojitegemea unahitaji yafanyike mambo yafuatayo:-

(a) **Elimu ya Kisasa**

Kwa vile uchumi wa kisasa unahitaji watenda kazi wenye ujuzi na maarifa ya sayansi na teknolojia ni lazima waandaliwe kwa kupewa elimu bora na ya kisasa. Msukumo wa elimu ya kisasa katika kipindi hiki utaendelea kuelekezwa kwenye:-

(a) Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, na Elimu ya Juu;
(b) Elimu ya Ualimu;
(c) Elimu ya Ufundi;
(d) Elimu ya Watu Wazima yenye manufaa.

(b) **Sayansi na Teknolojia:**

55. Chama Cha Mapinduzi kinaamini kuwa bila matumizi ya elimu ya sayansi na teknolojia nchi yetu haiwezi kuondokana na uchumi ulio nyuma na uchumi tegemezi kwa hiyo basi lazima yafanyike marekebisho katika mitaala ili mafunzo yanayotolewa yapate mwelekeo wa sayansi na teknolojia.

56. Hivyo, ili kuliwezesha taifa letu kujenga msingi wa uchumi wa kisasa unaotumia sayansi na teknolojia katika uzalishaji mali na utoaji huduma, Sera za CCM katika miaka ya 2010 hadi 2020, zitaendelea kusisitiza ujenzi wa misingi imara ya elimu ya Sayansi na Teknolojia kwa kuzingatia yafuatayo:-

(a) Serikali kutilia mkazo uwekezaji wa raslimali katika utafiti na kuufanya utafiti kuwa agenda ya kitaifa kwa kutenga asilimia moja (1%) ya pato ghafi la Taifa kwa ajili ya utafiti na maendeleo.

(b) Kusimamia taratibu za uhawilishaji wa teknolojia na utoaji hakimiliki kwa watafiti na wagunduzi.

(c) Kuhakikisha kwamba, matokeo ya utafiti na ugunduzi wa teknolojia yanawafikia walengwa wakiwemo wajasiriamali wakulima wadogo,

wa kati na wakubwa ili watumie matokeo hayo katika kuzalisha bidhaa bora zitakazoingia kwenye soko.

(d) Kuhimiza kupitia elimu yenye manufaa uelewa na matumizi ya Sayansi na Teknolojia katika nyanja zote za maisha ya wananchi mijini na vijijini ili wajenge utamaduni wa kuishi kisayansi.

(e) Kuhakikisha kwamba kila kituo cha utafiti kinakuwa shamba darasa kwa kutimiza malengo matatu yanayoshikamana ya: Utafiti, Maendeleo na Kuonyesha kwa mfano Matokeo ya Utafiti huo.

(f) Serikali kuishirikisha Sekta Binafsi katika kuchangia kwenye maendeleo na matumizi ya sayansi na teknolojia nchini.

(g) Serikali zifanye uhakiki wa uwezo wa kiteknolojia wa mitambo nchini ili kubaini fursa zilizopo na kuzitumia kwa ukamilifu.

(h) Ili tuwe na hakika kwamba nchi yetu itayafikia malengo ya dira ya 2020 na ya 2025, Serikali iandae programu mahusus ya kuandaa watalamu wa kada mbalimbali kama vile za uhandisi, uganga wa binadamu na wanyama, madini, jiolojia na kilimo watakaojaza nafasi muhimu na lazima katika kuyafikia malengo hayo ya dira.

(c) **Mapinduzi ya Kilimo**

57. Katika kipindi hiki Chama kitaendelea kuhamasisha na kuhimiza kilimo cha kisasa. Kilimo cha kisasa ndiyo ufunguo wa maendeleo ya uchumi wa Taifa na ndicho kitakachoongeza tija na ziada kubwa. Kilimo cha kisasa ndiyo kitakachoondoa hatua kwa hatua uchumi wa kujikimu na badala yake kujengeka uchumi wa soko wa kisasa.

58. Ongezeko la tija na ziada ya mazao litapunguza umasikini vijijini, na litaongeza mazao ya kuuza nje ili kujipatia fedha nyingi za kigeni na litachochea uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mazao. Aidha, litaongeza ukubwa wa mashamba, tija na ubora wa mazao yao.

59. Ili kufikia azma hii Mkakati wa Mapinduzi ya kilimo utalenga katika:-

(a) Kuwawezesha wakulima kutekeleza kanuni za kilimo bora ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao kwa kila ekari kulingana na viwango vya kisasa kwa kila zao wanalolima.

(b) Kuwawezesha wakulima kuongeza ukubwa wa maeneo wanayolima kwa kuanzisha mfumo wa kuwapatia mitaji pamoja na kuwakaribisha na kuwavutia wakulima wa kati na wakubwa.

60 Ili kufanikisha malengo haya Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali kutekeleza wajibu wake kwa kuipatia Sekta ya Kilimo bajeti stahiki na kufanya yafuatayo:-

(a) Kutilia mkazo suala la kueneza kilimo cha matrekta madogo na makubwa kwa Serikali kuhakikisha kwamba:-

(i) Bei ya matrekta madogo inakuwa ya chini nchini kote ili kuziwezesha familia kuyamiliki.

(ii) Serikali kusimamia uanzishwaji wa viwanda vya kuunganisha matrekta madogo hapa nchini.

(ii) Kuboresha mfumo wa upatikanaji wa pembejeo, masoko ya wakulima na kuhamasisha sekta binafsi na vikundi vya wakulima kutoa huduma ya pembejeo katika maeneo yao.

(iii) Kufufua na kuongeza vituo vya utafiti wa kilimo na kuendeleza utafiti shirikishi utakaowapatia wakulima fursa ya kutoa mawazo yao kuhusiana na matatizo yanayowakabili.

(iv) Kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji na kuhamasisha uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya miradi midogomidogo ya umwagiliaji.

(v) Kuondoa kodi zisizo za lazima hasa kwa zana na pembejeo za kilimo.

(d) **Mapinduzi ya Ufugaji**

61. Tanzania ina mifugo mingi lakini ufugaji wetu bado ni wa jadi, duni na unaojali zaidi uwingi kuliko ubora wa mifugo. Ng'ombe, mbuzi na kondoo pekee ni zaidi ya milioni thelathini, ng'ombe wakiwa nusu ya hao. Wanyama wanaofugwa wana kiwango kidogo cha ubora, wana uzito mdogo na wanatoa maziwa na ngozi hafifu.

62. Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2020 Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali zake kusimamia Mapinduzi ya ufugaji, ili uwe wa kisasa na kuongeza ubora wa ng'ombe wa maziwa na wa nyama.

63. Serikali kuandaa mpango kabambe wa kuwapatia wafugaji maji na malisho ya uhakika ili hatimaye Taifa liondokane na tatizo la wafugaji kuhamahama.

(e) **Mapinduzi ya Uvuvi**

64. Tanzania ina bahari, maziwa na mito yenye samaki wa aina nyingi. Hata hivyo bado wavuvi na taifa kwa ujumla halijafaidika na maliasili hii kwa sababu ya kutumia uvuvi wa jadi.

65. Katika kipindi hiki, Serikali chini ya uongozi wa CCM zitasimamia Mapinduzi ya sekta ya uvuvi kwa kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha ufugaji wa samaki, viwanda vya kusindika samaki, kuanzisha na kuendeleza vikundi vya wavuvi wadogo wadogo na kuwapatia mikopo na zana za kisasa. Serikali za Vijiji na Mitaa zitahimizwa kudhibiti uvuvi haramu na kuelimisha wananchi umuhimu wa hifadhi ya mazingira ya bahari, mito na maziwa. Aidha, suala la kuhamasisha uwekezaji wa ndani na wa nje kushiriki katika uvuvi wa bahari kuu litatiliwa mkazo.

(f) **Mapinduzi ya Viwanda**

66. Viwanda ni sekta kiongozi na chimbuko la modenaizesheni ya kilimo na uchumi kwa ujumla. Uchumi wa Viwanda una nguvu kubwa ya kuziwezesha sekta nyingine za Uchumi kuingia katika mkondo wa uchumi wa kisasa.

67. Sekta ya viwanda nchini bado ni ndogo na mchango wake kwenye pato la Taifa ni takribani asilimia kumi tu. Kutokana na ukweli huu katika kipindi cha 2010-2020 Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha kuwa Serikali zake zinasimamia uanzishwaji wa kujenga viwanda vidogo vidogo, Viwanda vya kati na viwanda vya msingi na kutilia mkazo viwanda vya kusindika na kuchakata mazao ya kilimo, mifugo na madini.

68. Katika kipindi cha Mwelekeo huu, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kuimarisha kifedha Benki ya Rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya viwanda kama mkakati wa kutumia kikamilifu uwezo wetu wa ndani wa kujitegemea.

69. Vile vile Chama kitazitaka Serikali kuwaandaa mabingwa katika fani mbali

mbali za sayansi na teknolojia ya Viwanda, watafiti na wagunduzi kwa kuishirikisha Tume ya Sayansi na Teknolojia, ili kuweka mtandao bora wa maendeleo ya viwanda nchini.

70. Chama kitazitaka Serikali kuandaa mpango utakaoishirikisha sekta binafsi katika kuanzisha na kuendeleza ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo ili kuyaongezea thamani katika soko na kuondokana na utamaduni wa kuuza mazao yetu yakiwa ghafi.

71. Wakati Taifa linawekeza zaidi katika kukuza Sekta ya Viwanda, Serikali zetu zibuni mkakati muafaka wa kulinda viwanda vyetu vichanga vilivyopo na vitakavyoanzishwa dhidi ya ushindani kutoka nje ambao usipodhibitiwa utaendelea kudhoofisha kukua kwa Sekta ya Viwanda nchini. Aidha, Chama kitazitaka Serikali kuandaa mpango wenye vivutio utakaoshirikisha sekta binafsi katika kuanzisha viwanda mama kwa kutumia rasilimali zilizopo za makaa ya mawe ya Mchuchuma, chuma cha Liganga na gesi ili kuharakisha maendeleo ya viwanda.

(g) **Miundombinu**

72. Sekta ya miundombinu inayojumuisha mawasiliano, ujenzi, uchukuzi na usafirishaji kwa njia ya barabara, maji na anga na utabiri wa hali ya hewa ni sekta ambayo huunganisha sekta nyingine zote za uchumi wa nchi na kuufanya uwe mfumo mmoja wa uzalishaji mali na utoaji huduma katika jamii. Uimara wa sekta hii na hasa kasi ya kukua kwake na kuenea katika maeneo yote ya uzalishaji mali na utoaji huduma ndicho kichocheo kikubwa siyo tu cha kukua kwa uchumi bali pia cha maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

73. Kwa kutambua umuhimu wa sekta hii, Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka kumi iliyopita kilizielekeza Serikali kuanzisha ujenzi mkubwa wa barabara za aina zote, madaraja, viwanja vya ndege na kununua vivuko mbalimbali kwa lengo la kuchochea ukuaji wa uchumi na kurahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa. Ujenzi wa daraja la mto Rufiji, Daraja la Umoja, Kivuko cha Kigamboni na wa barabara ya lami kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza ni mifano hai ya mafanikio makubwa ambayo yamepatikana.

74. Katika miaka kumi ya Mwelekeo huu, Chama kitaendelea kuzielekeza Serikali kutumia kipindi hiki kuhakikisha kwamba mafanikio yaliyopatikana yanalindwa na kupanuliwa zaidi kwa kutekeleza yafuatayo:-

    (a) Kuboresha, kuimarisha na kupanua mtandao wa reli nchini kwa kiwango cha kimataifa hususan Reli ya Kati, Reli ya TAZARA, Reli

ya Tanga/Arusha na kujenga reli mpya kwa lengo la kufungua huduma ya usafirishaji katika Kanda ya Mtwara, Kanda ya Kati kutoka Isaka kwenda Rusumo na Kanda ya Kaskazini kuunganisha Tanga na Musoma.

(b) Kuimarisha na kupanua mtandao wa barabara nchini hasa zile zitakazopita katika maeneo ya uzalishaji mkubwa wa kilimo na migodi pamoja na kukuza soko la ndani.

(c) Kuboresha na kuimarisha viwanja vya ndege vilivyopo nchini na kujenga vipya ili kuendeleza huduma ya usafiri wa anga.

(d) Kuboresha na kuimarisha miundombinu ya bandari zilizopo katika mwambao wa pwani na maziwa ili kuendeleza huduma ya usafiri wa majini ndani ya nchi yetu na nchi jirani.

(e) Kazi ya kukamilisha miundombinu ya usafirishaji wa umeme inayounganisha nchi yetu na nchi za jirani itakamilishwa. Hii itawezesha kuuza au kununua umeme kutoka nchi za jirani kutegemeana na mahitaji. Mradi mkubwa wa kuunganisha njia kuu ya umeme ya Zambia-Tanzania-Kenya itakamilika ili kuunganisha njia ya umeme na hususan biashara ya huduma hiyo baina ya nchi za Afrika ya Kaskazini, Mashariki na Kusini.

(f) **Nishati**

75. Maendeleo ya Uchumi wa Kisasa yanakwenda sambamba na matumizi ya nishati kwa mfumo mpana na endelevu, na ambao matumizi hayo yanapelekea ukuaji wa kiuchumi ambao unachangia uboreshaji wa kiwango cha maisha cha binadamu mmoja mmoja na hatimaye, uboreshaji wa maisha katika jamii yote.

76. Viwango vya ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa miaka kumi iliyopita vimeleta changamoto kubwa kwani ukuaji huo umesababisha mahitaji makubwa ya nishati kwa upande wa umeme kupanuka hususan kwenye maeneo ya mijini na vijijini na hivyo kusababisha ongezeko la wateja wanaoomba huduma hiyo. Vile vile kumejitokeza ongezeko la magari nchini ambalo limesababisha matumizi makubwa ya nishati ya mafuta na bidhaa nyingine zinazotokana na petroli.

77. Kwa kuzingatia haya, katika miaka kumi ijayo Chama Cha Mapinduzi kitazitaka Serikali kuhakikisha kwamba Sekta ya Nishati inachangia kwenye ukuaji na mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini kwa kuipunguzia TANESCO baadhi ya majukumu na kuishirikisha Sekta binafsi kubeba majukumu yaliyobaki. Hatua za makusudi zitachukuliwa kuzalisha umeme maeneo ya Stiegler's Gorge, Mchuchuma na kwingineko nishati kutokana na makaa ya mawe.

(b) Kukamilisha hatua ya kupeleka umeme kwenye makao makuu ya wilaya zilizobaki, kuandaa na kutekeleza mpango mkakati wa kupeleka umeme vijijini na Serikali kutenga uwezo wa ziada kwa kutambua mchango wa nishati hii katika maisha ya Mtanzania na mafanikio ya mipango ya maendeleo.

(c) Kuweka utaratibu wa kuingiza umeme kutoka nchi jirani ili kuongeza kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa umeme nchini.

(d) Nishati ya mafuta na masuala yote husika yanachangia mabadiliko ya mwenendo wa uchumi na maisha ya Mtanzania ya kila siku. Utafutaji wa mafuta na gesi asilia utaongezwa na TPDC itaongezewa uwezo ili kuharakisha upatikanaji wa mafuta na gesi asilia na matumizi ya nishati hizi ambazo kwa sasa zinaagizwa nje kwa gharama kubwa. Aidha, gesi asilia iliyopatikana sasa itaelekezwa kwenye uzalishaji wa umeme, mbolea, saruji na mafuta ya LPG ambayo ni mbadala wa mafuta ya Petroli na Dizeli, na kuongeza matumizi ya gesi asilia kama nishati ya majumbani. Sekta Binafsi itahimizwa na kupewa motisha na vivutio ili kushiriki katika miradi hii kwa mfumo wa PPP.

(e) Mwenendo wa matumizi ya nishati katika nyakati za sasa ni kuhimiza maendeleo ya nishati mbadala kama sehemu ya kuboresha na kutunza mazingira. Miradi ya nishati mbadala ya vyanzo vya rasilimali jua, upepo na joto ardhi itakamilishwa. Utafiti wa ndani utaboreshwa ili kuongeza matumizi ya nishati mbadala mashuleni, kwenye magereza ili kuongeza uzalishaji na matumizi ya vyanzo vidogo katika uzalishaji wa umeme na nishati mbadala za kupikia majumbani badala ya kuni na mkaa. Katika kufikia azma hii makampuni yenye uwezo wa kiuchumi na wa kitaaluma wa sayansi na teknolojia za kisasa yatapewa vivutio ili kuwezesha kushiriki na kuhaulisha matumizi ya nishati hizi katika maisha ya kila siku ya Mtanzania.

(g) **Madini**

78. Sekta ya madini ni kati ya sekta muhimu na zenye mchango mkubwa

kiuchumi na kijamii nchini. Katika miaka 10 iliyopita mapato yatokanayo na madini yamekua kila mwaka kutokana na mchango wa uchimbaji mkubwa ambao unafanywa nchini lakini pia kutokana na uchimbaji mdogo ambao unafanywa kwa kiasi kikubwa na Watanzania wa kipato kidogo.

79. Serikali imeandaa Sera na Sheria ambazo zimelenga kuongeza manufaa yanayotokana na sekta hii. Nia ni kuhakikisha uchimbaji mkubwa na uchimbaji mdogo unaoendelea uwe na manufaa makubwa zaidi kwa Taifa kiuchumi. Sera ya madini inatarajiwa pia iongeze uwekezaji wa uchimbaji wa kati ambao una nafasi ya ushiriki mpana zaidi. Uchimbaji mdogo unafanywa katika mazingira duni ya zana, mitaji, utaalamu wa kale, na masoko ya wachimbaji hawa siyo rasmi na hivyo hayatambui nguvu kubwa inayotumika kwenye uzalishaji na kwa kiasi kikubwa uchimbaji huu hauchangii kulipa kodi.

80. Aidha, pamoja na mchango mkubwa wa sekta ya madini, nchi yetu bado ina hazina kubwa ya madini ambayo haijachimbwa. Madini haya ni pamoja na Chuma, Nikeli, Makaa ya Mawe, Urani, Fosfeti; n.k. Madini haya yanaweza kuchimbwa na kuelekezwa kwa matumizi ya viwandani ama humu humu nchini au kwa kuuza nje ya nchi, na kwa madini kama makaa ya mawe na Urani yanaweza yakawa msingi wa kuongeza upatikanaji wa nishati. Serikali inadhamana kubwa ya kuhakikisha kwamba uchimbaji wa madini haya unaongeza uwezo wa Taifa kiuchumi kama sehemu mahsusi ya kujenga msingi wa modenaizesheni na kuongeza uwezo wa kiuzalishaji viwandani, lakini pia, kijamii kwa maana ya kwamba watu wengi zaidi wananufaika na ajira zenye maslahi na usalama zaidi kutokana na sekta hii. Pia, utaalamu wa uchimbaji madini na masuala mengine ya kijiolojia utapanua ushiriki wa Watanzania katika ajira ya migodini, badala ya kuwa na sehemu kubwa katika ajira za ujuzi mdogo.

81. Kwa kuzingatia haya, katika miaka kumi ijayo Chama Cha Mapinduzi kitaiagiza Serikali ihakikishe kwamba Sekta ya Madini inachangia kwenye ukuaji na mipango ya maendeleo, kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya Watanzania, kwa kufanya yafuatayo;

    (a) Uchimbaji mkubwa wa madini utasimamiwa na mikataba ambayo inahimiza ushiriki wa sekta ya Umma, na uwekezaji wa sekta binafsi nchini Tanzania. Kwa kuwa uwekezaji wa sekta ya madini ni mkubwa na huitaji mitaji mikubwa Serikali itahimiza ushiriki wa Sekta ya Fedha nchini, na taasisi za Umma ili kuhakikisha kuwa tunanufaika kwa kiasi kikubwa zaidi kimapato na uchimbaji huu. Aidha, taasisi na vyombo vya fedha vitaelekezwa kuwa na mfumo bora zaidi wa kukopesha au kuwezesha uchimbaji mdogo na wa

kati.

(b) Njia iliyo bora zaidi ya kuwasaidia wachimbaji wadogo ni kwa kuwahimiza kufanya shughuli zao katika utaratibu wa vikundi vya ushirika ili waweze kufikiwa kiuwezeshaji kwa mitaji, mikopo, na pia uwezeshaji wakitaalamu. Hii itawawezesha kuongeza matumizi ya zana na teknolojia za kisasa, kuwa na uzalishaji mkubwa zaidi kwa kutumia nguvu ndogo zaidi na katika mazingira ya usalama zaidi. Aidha, tatizo la masoko na uongezaji thamani madini litapatiwa ufumbuzi.

(c) Tatizo la ajira kwenye madini litawekewa mkakati wa kuboresha ushiriki wa Mtanzania kwa kuongeza nafasi za utaalamu wa masuala ya madini na jiolojia. Njia mojawapo ni kuboresha mitaala kwenye vyuo vya elimu ya juu na kuongeza ushiriki wa vijana wa Kitanzania. Hatua ya kuanzisha kitivo cha Taaluma za Sayansi za Ardhi cha Chuo Kikuu cha Dodoma na kukiunganisha na chuo cha Madini Dodoma ni moja ya mkakati utakaokamilishwa.

(d) Ukuaji wa Sekta ya Madini unaambatana na kuhitaji huduma husika kutoka kwenye sekta zingine kama vile usafirishaji, chakula, ulinzi, n.k. Serikali itahakikisha kwamba kama vile ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Madini pale ambapo huduma hizi zinapatikana nchini kwa kiwango stahili, kazi hizo zipewe makampuni ya Kitanzania.

(e) Kwa sababu ya upana wa sekta ya Madini na shughuli zake, usimamizi wa sekta hii ni sehemu muhimu ya kudhibiti mapato na ukwepaji kodi. Serikali itatakiwa iongeze uwezo wa taasisi za ukaguzi wa madini katika ngazi za utafiti na uchimbaji, na pia kuweka vivutio ili kupata uwekezaji katika kazi za kuongeza thamani.

(f) Suala la uharibifu wa mazingira litaongezewa mkazo ili kupunguza uharibifu wa mazingira lakini pia kuwawajibisha kisheria wale wote wanaofanya shughuli za uchumbaji usiozingatia utunzaji wa mazingira.

(h) **Utalii**

82. Tanzania ina utajiri mkubwa wa maliasili na historia ambavyo ni vivutio kwa watalii wa ndani na nje ya nchi. Sekta ya utalii imekuwa ikitoa mchango mkubwa katika ukuaji na upanuzi wa uchumi wa nchi yetu. Katika miaka kumi ijayo Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali zake kufanya yafuatayo:-

(a) Kuboresha mipango ya sekta ya utalii kwa kuwaongezea Watanzania fursa za kushiriki katika kutoa huduma kwa watalii.

(b) Kuimarisha utalii wa ndani ili kuwawezesha wananchi waone mazingira mema na maliasili za nchi yao.

(c) Kuwavutia watalii wa nje kwa kuboresha huduma na uzalishaji wa bidhaa zenye ubora kwa kutumia teknolojia rahisi na za kisasa ili ziwavutie watalii Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, hatua za kuvitangaza vivutio vya utalii nje ya nchi kwa njia ya tovuti zitaimarishwa.

(d) Kupanua uwezo wa kuwapokea watalii wengi zaidi kwa kuongeza kasi ya kuvutia ujenzi wa hoteli zenye mtandao wa juu na hadhi ya kimataifa na kuimarisha miundombinu ya barabara katika mbuga za wanyama na maeneo mengine yaliyo na vivutio vya utalii.

(e) Kuongeza udhibiti wa mapato ya utalii.

(f) Kuendeleza jitihada za kuhifadhi mazingira katika mbuga za wanyama, misitu, fukwe za bahari na maziwa ili kuvilinda na kuviendeleza kama mojawapo ya vivutio vya utalii.

(g) Kuimarisha utalii wa uwindaji nchini ili kuliongezea Taifa mapato.

(i) **Ardhi, Nyumba na Makazi**

83. Ardhi ni rasilimali namba moja katika ujenzi wa uchumi wa Taifa. Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2020, Sera za CCM zitaendelea kusisitiza suala la upimaji ardhi, mipango ya matumizi bora ya ardhi ngazi ya kijiji hadi Taifa, na umilikishaji ardhi wananchi kupitia mpango wa kurasimisha rasilimali za wanyonge (MKURABITA).

Kuhusu Ardhi

(a) Sera ya Taifa ya ardhi ya mwaka 1995 na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 zinafanyiwa mapitio ili ziendane na hali ya kiuchumi ya sasa, na kwamba elimu kwa umma kuhusu Sera na Sheria za ardhi hizo itaendelea kutolewa kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Miji.

(b) Kuhakikisha kuwa, Halmashauri za Miji na Wilaya zinajengewa uwezo na kuajiri wataalamu wa sekta ya ardhi na kupatiwa kazi na mafunzo yanayoendana na taaluma zao.

(c) Kuhakikisha kwamba, madaraka ya kusimamia sekta ya ardhi yanasogezwa karibu na wananchi (ugatuaji) katika ngazi za Kanda, Mkoa, Wilaya hadi vijijini.

(d) Utoaji wa Hatimiliki za Ardhi nchini unarahisishwa na kufanyika haraka ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kumiliki ardhi kisheria na kuwawezesha kutumia Hati hizo kupata mikopo katika vyombo vya fedha.

(e) Kupima mashamba ya wanavijiji na kuwapatia Hatimiliki za Kimila na kuhakikisha kwamba kila ofisi ya wilaya na kijiji inakuwa na masjala yake ya ardhi kwa ajili ya uhifadhi salama wa hati za ardhi.

(f) Kuanzisha Mfuko wa Kulipa Fidia ya Ardhi, ili kurahisisha ulipaji wa fidia mara Serikali inapotwaa ardhi kwa ajili ya manufaa ya umma .

(g) Kuboresha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na kuanzisha mapya katika kila Wilaya na hasa Wilaya zenye migogoro mingi ya ardhi.

Kuhusu kuboresha Makaazi Mijini na Vijijini

(a) Kuhakikisha kuwa, mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi unatekelezwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

(b) Kuongeza kasi ya kutekeleza mpango wa upimaji wa viwanja na mpango miji, kwa kipaumbele katika maeneo yanayokua kwa kasi, likiwemo Jiji la Dar-es-Salaam, Majiji na Miji mingine nchini. Huu ndio wakati kwa nchi yetu kupata uwezo wake yenyewe wa kupima ramani ya nchi nzima.

(c) Kuanzisha Mji wa kisasa wa Kigamboni,pamoja na Miji, midogo nje ya Miji mikubwa kwa lengo la kupunguza msongamano katikati ya Jiji na Miji.

(d) Kuhakikisha kuwa, Makaazi yaliyojengwa kiholela (slums) katika kila miji yanarasimishwa na wananchi wanapatiwa Leseni za Makaazi na Hatimiliki, na pia kuyawekea miundombinu muhimu kama barabara, mifereji ya maji ya mvua, taa za barabarani n.k.

Kuhusu Maendeleo ya Nyumba:

(a) Kufanya tafiti mbalimbali za vifaa vya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu kwa ajili ya wananchi wa kipato cha chini, na kuwahamasisha wananchi kuanzisha vikosi vya ujenzi wa nyumba bora na zenye gharama nafuu na kujiunga katika Ushirika wa Ujenzi wa Nyumba Nchini.

(b) Kuhakikisha kuwa Shirika la Nyumba la Taifa, linakuwa mwendelezaji ardhi mkubwa (Master Estates Developer) anayejenga nyumba kwa ajili ya kuuza au kupangisha kwa makundi yote ya wananchi, na hasa wenye kipato cha chini na kati.

(c) Kuanzisha mpango wa ujenzi shadidi wa miji (vertical) badala ya ujenzi tandavu wa sasa ili kutumia ardhi vizuri, kupunguza gharama za kuweka miundombinu, mijini na pia kupendezesha miji kwa majengo ya ghorofa.

(d) Kuimarisha mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba nchini , ikiwa ni pamoja na kuyahamasisha mabenki na vyombo vingine vya fedha, ili kutoa mikopo ya muda mrefu na yenye riba nafuu.

Kuhusu Upimaji na Ramani

(a) Kutunga na kupitisha Sera ya Upimaji na Ramani, na kuandaa mikakati ya utekelezaji wa sera hiyo.

(b) Kuhakikisha kuwa, vijiji vyote nchini vinapimwa ili kuonyesha wazi wazi maeneo ya uwekezaji na kuanzishwa Hazina ya Ardhi kwa lengo la kuharakisha upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

(c) Kuhakikisha kuwa kasi ya upimaji wa viwanja na mashamba nchini inaongezeka kwa kuwahamasisha wananchi kuchangia gharama za upimaji na kwa kutumia wapimaji binafsi waliosajiliwa kisheria.

(d) Kuhakikisha kuwa upatikanaji wa ramani za msingi nchini unarahisishwa kwa lengo la kuharakisha upimaji wa ardhi kwa kuanzisha kituo cha kupokea picha za satelite na pia kujenga alama za upimaji wa ardhi zinawekwa nchi nzima, ili kurahisisha utayarishaji wa ramani na upimaji wa ardhi nchini.

(e) Kuhakikisha kuwa Halmashauri za Miji na Wilaya zinajengewa uwezo wa kupima viwanja na kuuza kwa wananchi kupitia mfuko wa kuzungusha fedha za kupima viwanja (Plot Development Revolving Fund).

SURA YA TATU

UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI

84. Chama Cha Mapinduzi katika sera zake za msingi kama zilivyoainishwa katika Mwelekeo wa Sera za CCM katika Miaka ya Tisini na Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000-2010, kimetamka bayana kwamba, mkakati mkuu wa uwezeshaji wa kiuchumi wa wananchi ni ule unaohakikisha kwamba wananchi wenyewe wanamiliki na kuendesha uchumi wa nchi yetu ama mmoja mmoja kwa kupitia vyama vyao huru vya ushirika wa aina mbalimbali au kwa kupitia makampuni ya wananchi ya ubia ambamo maelfu ya wananchi watanunua hisa na kwa kupitia umilikaji wa dola kwa mashirika yote yatakayoendelea kuwa mikononi mwake.

    Katika kipindi cha miaka ya 2010-2020 jukumu kubwa la Chama Cha Mapinduzi litakuwa kuhakikisha kuwa mkakati huu unaendelea kutekelezwa kwa nguvu zaidi kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:-

Mafunzo ya kuwawezesha wananchi kiuchumi

85. Elimu na Ujuzi ndivyo vitokavyowawezesha wananchi kushiriki katika ujenzi wa msingi wa uchumi wa kisasa. Wakati huo huo, Watanzania wenye vipaji wataandaliwa katika fani za uongozi wa uchumi na kuwasaidia watu ambao wako tayari kuthubutu kuchukua hatua za kiuchumi. Kuthubutu kiuchumi ndiyo chimbuko la msukumo katika uchumi wa kisasa. Chama Cha Mapinduzi, kwa kupitia Serikali zake, kitaendelea kuwapa wananchi elimu na mafunzo juu ya menejimenti ya aina mbalimbali za uchumi wa kisasa.

Ushirika kama Chombo cha Uwezeshaji

86. Ushirika ndicho chombo kikuu cha kuwaunganisha wananchi na kuwapa nguvu ya kutetea maslahi yao na kujiendeleza. Katika kilimo, ufugaji na uvuvi, ushirika ni chombo cha kuwapatia mtaji kutokana na michango na ushuru, njia ya uhakika ya kufikisha mazao kwenye masoko, kuwafikishia pembejeo na zana za kisasa. Aidha, ushirika ni mkondo wa kueneza elimu

ya ushirika na elimu ya uzalishaji bora kwa wanachama wake.

87. Katika kipindi hiki mkazo utaendelea kuwekwa kwenye kujenga ushirika wa vyama vya msingi ili kuwasaidia wakulima, wafugaji na wavuvi kuondokana na umaskini. Wananchi wengi zaidi wataendelea kushawishiwa na kuhamasishwa wajiunge na ushirika huu. Wana CCM kama askari wa mstari wa mbele watatakiwa kuonyesha mfano.

88. Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kutoa msukumo mkubwa juu ya elimu ya ushirika na juu ya manufaa ya ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS) katika kuwapatia wahusika mtaji ili waweze kushiriki katika uwekezaji nchini.

Mifuko ya mikopo ya kuwawezesha wananchi Kiuchumi

89. Serikali, chini ya uongozi wa CCM, zitaendelea kuboresha urataribu wa mikopo kwa wanawake, vijana na wafanyabiashara wadogo. Serikali za Mitaa zitaendelea kuhimizwa kutenga asilimia 10 ya makusanyo yao kwa ajili ya mikopo ya wanawake na vijana. Serikali Kuu itaongeza kiwango cha fedha inazotenga kwa ajili ya mikopo na kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatolewa kwa mtiririko wa uhakika.

90. Baadhi ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs) yameonyesha kuwa na uwezo wa kuwawezesha wajasiriamali katika kujiendeleza kiuchumi. Katika miaka kumi ijayo Serikali zitatakiwa kuzisimamia NGOs kwa karibu zaidi ili ziweze kushiriki kwa ukamilifu katika kuwawezesha wajasiriamali kupanua shughuli zao za kiuchumi.

Vyombo vya Fedha na Benki za Wananchi

91. Katika kipindi hiki Chama Cha Mapinduzi kitazitaka Serikali kutoa msukumo mkubwa katika kuanzisha vyombo vya fedha vyenye lengo la kutoa mikopo ya muda mrefu na riba nafuu ya kuwawezesha wananchi kuingia katika miradi ya kisasa ya kilimo, ufugaji, uvuvi na viwanda. Mabenki mengi tuliyonayo sasa kwa aina ya shughuli zao ni mabenki ya kibiashara zaidi kuliko yale ya kuendeleza sekta za uzalishaji mali hususan kilimo. Aidha, hutoza riba kubwa. Hivyo ni muhimu Serikali zikahakikisha kuwa kwa makusudi vinaanzishwa vyombo vya fedha ambavyo vitasaidia kuwawezesha wananchi kwa riba nafuu kuliko ilivyo sasa, ikilenga uanzishwaji wa Benki ya Kilimo, Benki ya Kuendeleza Viwanda na Benki ya kutoa mikopo ya muda mrefu ya ujenzi wa nyumba.

92. Wananchi wataendelea kuhamasishwa ili waanzishe Benki za Wananchi

katika mikoa kwa sababu kuanzishwa kwa benki hizo kunaunda mazingira mazuri ya kuchochea maendeleo yao.

93. Katika kipindi cha miaka 10 ijayo, CCM itazitaka Serikali kutoa kipaumbele kwenye matumizi ya mikopo na karadha, mikopo ya nyumba na umilikishaji sehemu ya nyumba kama njia kubwa ya kuwawezesha wananchi.

Mpango wa Kuwawezesha Wasomi Kujiajiri

94. Kwa mtazamo mpana wa Sera ya Uwezeshaji Kiuchumi, aina ya kwanza ya uwezeshaji ni ile ya mtu mwenyewe kujiwezesha. Yaani mtu anajiwezesha pale anapotambua vipaji alivyonavyo na anaamua kujituma kwa kuvitumia vipaji hivyo.

Kwa ujumla elimu yetu hadi hivi sasa imeegemea kwenye kuelimisha watu ili waajiriwe au watumwe. Lazima sasa elimu tunayoitoa kwa vijana wetu ijielekeze kwenye kuandaa watu wenye kujituma. Wanaojiajiri ni watu wanaojituma.

95. Kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali sasa tuna wanafunzi wengi shuleni na katika vyuo vya elimu ya juu. Matokeo yake ni kuwa kuna vijana wengi wanaomaliza masomo ya sekondari, ya vyuo na hata vyuo vikuu (pamoja na VETA) lakini hawapati kuajiriwa kwa sababu uchumi wetu haupanuki kwa haraka kiasi hicho. Hivyo jambo jema la nchi kuwa na watu wengi, vijana wengi waliosoma vizuri sasa limeanza kuwa tatizo kwa nchi.

96. Kuwa na vijana wengi waliosoma ni nguvu kubwa kwa Taifa. Ili Taifa liweze kuitumia nguvu hii kwa maslahi ya vijana wenyewe na kwa maendeleo ya kiuchumi na jamii ya nchi yetu, CCM itazitaka Serikali kuibua Mpango Kabambe wa kuwawezesha kiuchumi vijana wasomi waliotayari kujituma kwa kujiajiri ili watumie nguvu na maarifa waliyonayo katika kilimo, ufugaji, uvuvi n.k. wa kisasa. Mpango huu unawezesha vijana hawa kwa:-

(a) Kuwaandalia na kuwapa mafunzo ya ujasiriamali na yanayohusu shughuli wanazokusudia kuzifanya.

(b) Kuweka utaratibu mwepesi wa kupata mikopo nafuu.

(c) Serikali kutenga maeneo makubwa ya ardhi kwa ajili ya mpango wa aina hii kwenye maeneo karibu na miji, majiji na kwingineko.

(d) Watakaoshiriki katika mpango huu washauriwe kuunda chombo chao cha kushauriana.

97. Utaratibu wa aina hii wa kuwawezesha wasomi na wataalamu **kujiajiri** una manufaa mawili kwa Taifa:-

(a) Unatoa ajira ya uhakika kwa wahusika hivyo kuipunguzia nchi tatizo la watu kukosa ajira na madhara yake, na

(b) Unawezesha wasomi kutoa mchango chanya katika kujenga uchumi wa kisasa na kuongeza utajiri wa nchi.

98. Aidha, Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali kuwa na mpango unaohusu Sekta ya Ujenzi kwa:-

(a) Kubuni mpango utakaowawezesha wahandisi wanaohitimu katika fani mbalimbali kujiajiri ili washiriki katika kuharakisha katika ujenzi wa nchi.

(b) Mpango huo pia uweke utaratibu wa kuyawezesha makampuni ya Makandarasi Watanzania kuboresha uwezo wao wa kitaaluma ili wapande ngazi na kuweza kushindana kwenye zabuni za kimataifa nchini na nje.

99. Katika kutekeleza mikakati ya kuwawezesha wananchi kiuchumi Vijana na Wanawake watapewa kipaumbele.

Nafasi ya Dola katika Kusimamia Sera ya Uwezeshaji

100. Katika kipindi cha miaka kumi ijayo (2010-2020) sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi itatekelezwa kwa kuhakikisha kuwa Serikali kwa makusudi inaweka mikakati ya uwezeshaji itakayolenga katika kuendelea kuwainua wananchi wa kawaida bila kuwasahau wananchi wa kati na wakubwa. Wajasiriamali wote wa chini, kati na wakubwa watawekewa mikakati itakayowapa fursa ya kuzalisha mali au kutoa huduma kwa kuzingatia soko na kwa wawekezaji kutoka nje kuingia ubia na Watanzania hasa wale wenye ujuzi na taaluma lakini hawana mitaji.

Upendeleo kwa Wananchi katika Ajira na Biashara

101. Katika kipindi hiki wajibu mkubwa wa Serikali utakua ni kuhakikisha kuwa nafasi ya kwanza ya ajira na biashara nchini iwe imetengewa Watanzania. Pale tu ambapo hakuna Watanzania wenye elimu na uwezo wa kuimudu

kazi hiyo ndipo wageni wafikiriwe. Changamoto kubwa katika kutekeleza azma hii ni Watanzania wenyewe kuwa na sifa zinazowawezesha kushindana na kulikamata soko la ajira. Na hapa ndiyo maana suala la elimu linakuwa ni la msingi sana.

102. Vile vile katika biashara sehemu kubwa ya zile za reja reja zinaweza kufanywa na Watanzania wenyewe. Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali zake kufanya jitihada na dhamira za makusudi kuwainua na kuwajengea uwezo Watanzania ili waweze kushindana katika soko la ndani badala ya kuwaachia wageni.

103. Wakati umefika wa kuweka mazingira bora ya upendeleo kwa Watanzania, kama inavyofanyika katika nyanja za kimataifa kwa mfano katika utoaji wa kandarasi za ujenzi, manunuzi n.k. Kuwapendelea Watanzania katika Ajira na biashara nchini ni njia mojawapo ya kuwawezesha kiuchumi ili mradi elimu iwawezeshe kupata upendeleo huo.

104. Katika kutekeleza Sera hii ya upendeleo kipaumbele kitatolewa kwa Wanawake na Vijana.

SURA YA NNE

KUTUMIA FURSA ZA KIJIOGRAFIA ZA NCHI YETU KUSUKUMA MAENDELEO

105. Tanzania ni nchi yenye fursa nzuri ya kijiografia ambayo inaweza kutoa mchango mkubwa katika kujenga uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea na kuwawezesha wananchi kiuchumi endapo itatumia eneo la bahari kuwa lango kuu kwa watu na mizigo kuingia na kutoka katika ukanda wa nchi za Afrika Mashariki na Kati ambazo hazina bahari.

106. Kwa maumbile yake Tanzania inapakana na nchi ya Malawi, Zambia, Burundi, Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), ambazo hazina bandari na kutegemea kwa kiasi kikubwa kupitisha bidhaa na watu bandari za Tanzania.

107. Kuwepo kwa Bandari ya Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Zanzibar, Kasanga, Kigoma na Mbambabay kunaipa Tanzania nafasi na mazingira maalumu ya kijiografia ambayo ni nyenzo muhimu ya kiuchumi. Kwa hiyo bandari zetu lazima ziimarishwe ili ziweze kuwa kivutio kwa majirani zetu.

108. Ili mazingira haya ya kijiografia yawe na manufaa kwa maendeleo ya kiuchumi, Chama Cha Mapinduzi kitazitaka Serikali zake kuandaa na kutekeleza mpango kabambe wa kufungua **lango kuu** kwa kujenga miundombinu mipya na kuimarisha iliyopo hususan, bandari, reli, barabara na viwanja vya ndege ili iweze kukidhi mahitaji ya kiuchumi ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

SURA YA TANO

SEKTA YA HUDUMA ZA JAMII

109. Chama Cha Mapinduzi kina lengo la kusukuma ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kwa kuzingatia rasilimali watu na rasilimali za nchi zilizopo.

110. Ubora na ustawi wa huduma za jamii hutegemea ni kiasi gani cha ziada inayozalishwa nchini hutengwa kwa ajili ya kugharamia huduma hizo. Hadi sasa hatua kubwa za mafanikio zimefikiwa Tanzania Bara na Zanzibar katika kutoa huduma za elimu, afya na maji. Katika mchakato wa kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Tanzania inayojitegemea, Chama kitaendelea kuzielekeza Serikali zake kutoa kipaumbele stahiki kupitia bajeti za kila mwaka kwa **maendeleo** na **uimarishaji** wa elimu, afya na maji nchini kote.

Huduma za Elimu

111. Ili uchumi wa kisasa nchini uweze kujengwa na watu walio tayari kujifunza na kutumia maarifa ya kisasa ni lazima elimu ipewe kipaumbele cha kwanza na serikali zetu. Kwa maana hiyo vipaumbele vifuatavyo vitazingatiwa:-

(a) Kuhakikisha kwamba kila shule ya msingi ina darasa la Elimu ya Awali lenye mahitaji muhimu ya watoto.

(b) Kuhakikisha kwamba kila shule ya msingi na ya Sekondari ina walimu, vitabu na miundombinu ya kutosha. Aidha, miundombinu ya sayansi itaimarishwa zaidi.

(c) Kwa kuzingatia upungufu wa waalimu hasa wa sayansi na hisabati, Serikali itahimizwa kuzingatia utaratibu wa elimu masafa kwa kutumia mtandao wa kompyuta hasa kwa masomo ya sayansi na teknolojia.

(d) Kuandaa mkakati wa kuwahamasisha, kuwashawishi na kuwawekea vivutio vya kuwafanya vijana wapende kusoma masomo ya sayansi.

(e) Kuhakikisha kuwa maslahi ya walimu yanazingatiwa hususan usafiri

na ujenzi wa nyumba za kutosha za walimu katika shule zote za msingi na sekondari ili kuboresha zaidi mazingira ya utoaji wa elimu nchini. Aidha, katika shule za sekondari za Kata, ujenzi wa mabweni ya wanafunzi hasa wasichana utaendelezwa.

(f) Serikali zitawadhibiti wale wote wenye tabia ya kuvamia maeneo ya mijini na vijijini yaliyotengwa kwa ajili ya mazingira ya shule.

(g) Kuongeza juhudi za kutengeneza madawati katika shule zote ili kuboresha mazingira ya ufundishaji.

(h) Serikali zitatakiwa kurekebisha Mitaala ya Elimu ya Sekondari na ya Mafunzo ya Walimu kwa kuzingatia elimu ya kujitegemea katika fani mbalimbali ili vijana wanaomaliza masomo yao waweze kutumia elimu waliyoipata katika kujitegemea.

(i) Katika kipindi hiki cha miaka kumi ijayo, Serikali itatakiwa kuchukua hatua ya kubaini na kutaja wazi wazi kitabu cha kiada cha kila somo kwa shule za msingi na za sekondari.

(j) Kuboresha mafunzo ya Ualimu kwa kuhakikisha kwamba kila mwalimu wa shule ya msingi anaandaliwa kufundisha masomo mawili tu anayoyamudu pamoja na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA).

(k) Utaratibu wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu utatazamwa upya kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa mikopo hiyo kwa wanafunzi wote wenye sifa za kudahiliwa chuoni.

(l) Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania zitatoa fursa za taaluma ambazo zitavutia wanafunzi, wahadhiri na watafiti kutoka ndani na nje ya nchi yetu.

Huduma ya Afya

112. Moja ya maeneo muhimu ya huduma za jamii ni uimarishaji wa afya za wananchi wetu mijini na vijijini. Katika kipindi hiki mkazo utawekwa katika kuimarisha, kuboresha na kuendeleza mafanikio ambayo yamepatikana kwa kuzingatia yafuatayo:-

a) Kutekeleza kwa ukamilifu Mpango wa

Maendeleo ya Afya ya Msingi wa miaka 10 ambao unasisitiza zaidi Mkakati wa Kinga katika utoaji wa huduma ya afya nchini, kuimarisha huduma ya afya ya mama na mtoto na mpango wa uzazi salama.

b) Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na ukaguzi wa huduma za afya na ustawi wa jamii nchini kote ili kuhakikisha kwamba huduma bora zinatolewa kuanzia ngazi ya hospitali ya rufaa hadi zahanati ya kijiji.

c) Kuweka utaratibu muafaka utakaowawezesha wagonjwa wengi kutibiwa popote walipo chini ya Mfuko wa Bima ya Jamii kwa kuzingatia makundi mbalimbali ya wananchi yatakayoainishwa. Aina zote za magonjwa ya kawaida yatatibiwa chini ya mfuko huu.

d) Kuimarisha mfuko wa Afya ya Jamii (Community Health Fund) katika kila wilaya na kuweka utaratibu muafaka utakaowezesha wagonjwa kutibiwa chini ya mfuko wa Bima ya Jamii kwa kuzingatia makundi mbalimbali ya wananchi yatakayoainishwa.

e) Kuimarisha programu za utafiti na utengenezaji wa dawa nchini badala ya kutegemea watu wa nje ambao malengo yao siyo sawa na yetu.

f) Kupanua sana mafunzo ya wataalamu wa afya wa aina na ngazi mbali mbali kwa kutumia vifaa vya teknolojia ya kisasa.

g) Kutekeleza lengo la kuziongezea uwezo hospitali za Mikoa kuwa hospitali za rufaa kwa kuzipatia vifaa, wodi za wagonjwa, wataalamu na dawa. Katika zoezi hili, Muhimbili ifanyike kuwa Hospitali ya Taifa yenye uwezo wa hali ya kimataifa katika kutibu magonjwa.

h) Kuboresha maslahi ya watumishi wa sekta ya

afya katika ngazi zote.

i) Serikali zitawahamasisha wadau wengine waendelee kuchangia gharama za afya kwa hali na mali.

j) Serikali zitatakiwa kuweka mkazo mkubwa katika suala la upatikanaji wa kutosha wa vifaa vinavyohitajika wodini wakati wa kujifungua kwa mama wajawazito ili huduma hiyo itolewe bure kwa wanawake wote.

k) Kuendelea kuboresha huduma za matibabu kwa wazee wote nchini.

l) Kuendelea kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za afya nchini.

m) Kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu na milipuko ya magonjwa ya hatari.

Huduma za Maji

113. Kutokana na utekelezaji wa Sera ya Maji ya mwaka 2002 ambao unaendelea, mafanikio makubwa yamepatikana hadi sasa. Kupitia Mwelekeo huu wa Sera, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuitaka Dola itekeleze mambo yafuatayo:-

a) Kuimarisha usambazaji na ugawaji wa rasilimali za maji kwa kuzingatia matatizo ya maeneo. Hii ni pamoja na kudhibiti mianya yote ya upotevu wa maji kwa kuimarisha ukaguzi wa miundombinu ya maji.

b) Kukamilisha maandalizi na kutekeleza Sera ya Maji na sheria yake itakayozitaka wizara zote, viwanda, vyuo, taasisi, hoteli na watu binafsi watakaojenga nyumba za kisasa mijini na vijijini kujenga miundombinu ya kuvuna maji ya mvua.

c) Kuimarisha uwezo wa ofisi za maji za mabonde yote tisa na maabara za maji ili kuboresha huduma ya maji katika mabonde hayo ambayo ni ya mito

Pangani, Rufiji, Wami/Ruvu, Bubu na Ruvuma; Maziwa ya Victoria, Nyasa, Rukwa na Tanganyika na Bonde la Kati (Ziwa Eyasi na Manyara).

d) Kuboresha huduma ya maji katika miji mikuu ya mikoa, wilaya na miji midogo kwa kukarabati na kujenga miundombinu ya majisafi na majitaka.

e) Kuimarisha na kuboresha zaidi mkakati wa kilimo cha umwagiliaji maji ili ifikapo mwaka 2020, karibu nusu ya mazao ya chakula chetu yaweze kutokana na kilimo hicho. Sekta binafsi itahamasishwa kushiriki kwa ukamilifu katika kilimo cha umwagiliaji maji.

f) Kuendeleza juhudi za upimaji wa maji ardhini na uchimbaji wa visima katika wilaya zenye uhaba wa maji safi na salama ili kukuza asilimia ya wananchi wa Vijijini wanaopata huduma hiyo.

g) Kuweka msukumo mkubwa katika uchimbaji wa malambo/mabwawa ya maji katika maeneo ya wafugaji kwa kukinga maji mengi ya mvua kwa ajili ya mifugo ili kuzuia uhamaji wa wafugaji wa ng'ombe.

h) Kuendelea kuwaelimisha wananchi washiriki katika kumiliki, kutunza na kuendesha miradi ya maji iliyopo katika maeneo yao. Wahimizwe pia kulinda vyanzo vya maji katika maeneo yao ili visikauke kutokana na uharibifu wa mazingira.

i) Maji ni uhai na pia maji ni afya. Hivyo Serikali ihakikishe kwamba mamlaka za maji zinaendeshwa kwa gharama nafuu ili watumiaji wa maji wasibebeshwe gharama zisizo za lazima ambazo ni kero kwa wananchi.

(k) Kuhakikisha kuwa mitaji na rasilimali zilizotumika katika kuwapatia wananchi wengi huduma hazipotei bure kutokana na ukosefu wa ukarabati wa miradi hiyo. Hivyo Chama kitazitaka Serikali kuhakikisha kuwa miradi yote mikubwa inayotoa na kusambaza maji kwa watu wengi inatengewa fedha za ukarabati badala ya kuingiza programu mpya za maji.

SURA YA SITA

UTAWALA BORA, DEMOKRASIA NA MADARAKA YA WANANCHI

114. Baada ya Mafanikio makubwa ya kubadili mfumo wa Chama kimoja na kuingia mfumo wa vyama vingi vya siasa, kazi iliyofanywa kwa ufanisi mkubwa katika miaka ya tisini, Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha 2000 hadi 2010 kimeendelea kuimarisha misingi ya demokrasia kwa kuhakikisha kuwa shughuli zote za kisiasa zinawashirikisha wananchi wote kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi bila kuacha mianya ya kujengeka kwa udikiteta wa aina yoyote. Kutokana na kazi hii nchi imeendelea kuwa na amani na utulivu, hali ambayo imechangia kwa kiwango kikubwa kuchochea maendeleo ya kiuchumi kwa kuruhusu uwekezaji wa rasilimali katika mazingira ya utulivu.

115. Katika kipindi cha miaka kumi ijayo (2010-2020) Chama Cha Mapinduzi

kitaendeleza jitihada zake za kuimarisha Utawala Bora kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kuona kwamba Serikali wakati wote inaendeshwa kwa kuheshimu na kuzingatia Utawala wa Sheria, yaani Katiba ya Nchi, Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo na ambazo zinaweza kutungwa na kukidhi haja ya wakati uliopo.

(b) Kuhakikisha kwamba Serikali inasimamia utekelezaji wa Maadili ya Viongozi kwa dhati ili kuimarisha Utawala Bora.

(c) Kuhakikisha kwamba Serikali zinazingatia uwazi katika kuendesha masuala ya nchi, kuimarisha usimamizi wa matumizi mazuri ya fedha na rasilimali za umma; uadilifu katika utendaji kwa kuzingatia misingi ya sheria; uwajibikaji na kuendeleza utamaduni uliojengeka nchini wa kubadilisha uongozi wa juu wa nchi kwa amani na mshikamano kwa faida ya Taifa letu na kukamilisha zoezi la kuzipitia upya sheria zinazogongana kwa lengo la kuimarisha demokrasia na Utawala Bora katika jamii.

(d) Kuona kwamba Serikali zinaboresha mara kwa mara mishahara ya wafanyakazi wa umma ili viwango vyake vizingatie ukuaji wa uchumi wa Taifa na hali halisi ya maisha ya kila siku.

Maadili

116. Dhana ya maadili ni pana na inajumuisha mambo mengi yanayoigusa jamii yakiwemo matumizi ya madaraka ya umma, uwajibikaji, utii wa sheria za nchi, uaminifu, uadilifu, uzalendo na kupenda kazi, tabia na mwenendo wa kila mwananchi. Ili kuimarisha maadili mema na ustawi wa Taifa letu kiuchumi, kijamii na kiutamaduni katika kipindi cha utekelezaji wa Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2010-2020, Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha kuwa Serikali inachukua hatua thabiti za kusimamia maadili mema na kuifanyia mapitio sheria ya maadili ya viongozi ili kuondoa mapungufu yote yaliyopo.

Vita Dhidi ya Rushwa

117. Vita dhidi ya rushwa ni mkakati endelevu wa utekelezaji wa kiapo cha mwanachama wa CCM, kwamba **rushwa ni adui wa haki na kwamba mwana-CCM hatapokea wala kutoa rushwa**.

118. Rushwa ni kikwazo cha maendeleo na pia ni kikwazo kikubwa cha utoaji wa haki nchini. Kwa kuzingatia uzito wa tatizo hili, Serikali katika miaka kumi ijayo ya Mwelekeo huu, zitaendeleza mapambano yaliyokwishaanza kwa kuchukua hatua madhubuti dhidi ya rushwa kwa kuwashirikisha wananchi na kuimarisha vyombo vya kupambana na rushwa.

Serikali za Mitaa

119. Serikali za Mitaa ni chombo cha wananchi cha kuwashirikisha katika utawala wa nchi. Pamoja na juhudi za makusudi zilizofanyika katika vipindi vilivyopita za kuimarisha uhusiano baina ya Madiwani na Watendaji na baina ya Halmashauri na wananchi, Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka kumi ijayo kitazielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuimarisha uhusiano wa Serikali za Mitaa, Madiwani, Watendaji, wananchi na makundi mbalimbali ya kijamii kwa manufaa ya maendeleo ya wananchi.

(b) Kuendelea kuziimarisha Serikali za Mitaa ili ziwe kitovu cha kusukuma maendeleo, kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuimarisha madaraka ya wananchi.

(c) Kuendelea kuziimarisha Serikali za Mitaa kifedha na kiutaalamu ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu na kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi mkubwa zaidi.

(d) Kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kutupia taka za mjini (dampo) na kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kutenganisha taka ngumu na nyinginezo ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

(e) Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vinavyotumia taka ngumu kama malighafi ya kuzalisha umeme na bidhaa mbalimbali.

Vyombo vya Habari

120. Vyombo vya habari ni sekta muhimu katika kuwaelimisha wananchi juu ya masuala mbalimbali yanayotokea nchini na duniani na kuimarisha demokrasia. Chama katika kipindi kilichopita kimeendelea kuhakikisha kwamba Serikali zinalinda uhuru wa vyombo vya habari na wa wananchi katika kupata habari sahihi kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa. Hadi mwishoni mwa mwaka 2009 jumla ya magazeti 91 yamesajiliwa kati yake 16 huchapishwa na kutolewa kila siku. Aidha, vituo

vya redio 58 na vya televisheni 28 vimeanzishwa nchini kote.

121. Katika kipindi cha miaka kumi ijayo bila ya kuathiri uhuru wa vyombo vya habari Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kufanya mapitio ya sheria ya vyombo vya habari ili kuondoa mianya inayosababisha ukiukwaji wa maadili ya uandishi wa habari na kuweka ada na dhamana ya uanzishaji wa vyombo vya habari.

(b) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Habari na Sera ya Utangazaji zinazohimiza upanuzi wa uhuru wa habari na kuongeza idadi ya vituo vya utangazaji vikiwemo vya watu binafsi.

(c) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Habari na Sheria ya Utangazaji kwa kuratibu mabadiliko ya mfumo wa urushaji wa matangazo ya dijitali na kuhakikisha kiwango kinachotegemewa kinafikiwa.

Jumuiya na Asasi za Kijamii

122. Chama Cha Mapinduzi katika vipindi vyote vya mabadiliko ya kisiasa kimeendelea kuunga mkono nafasi ya jumuiya na asasi za kijamii zikiwemo za kiuchumi kama vile vyama vya wafanyabiashara na za kitaaluma kama vile walimu, madaktari, wahandisi, waandishi wa habari au za kijamii kama vile za wanawake, vijana, na vikundi vya maendeleo vya wananchi. Jumuiya hizi zote zina nafasi muhimu katika kuimarisha demokrasia ndani ya umma na kuharakisha maendeleo ya wananchi.

123. Katika kipindi hiki kijacho cha 2010-2020 Chama Cha Mapinduzi kwa kushirikiana na Serikali itakazokuwa inaziongoza kitaendelea kupanua wigo wa wananchi kujiletea maendeleo yao kwa kutumia makundi mbali mbali kwa mujibu wa sheria na bila ya kuathiri mshikamano wa kitaifa na kufanya mapitio ya sheria ya usajili na kusimamia uendeshaji wa asasi hizo ili kuimarisha uwajibikaji wake kwa wananchi.

Vyama vya Wafanyakazi

124. Katika mfumo wa uchumi wa soko, Serikali inajiondoa kwa kiwango kikubwa kama mwajiri mkuu. Katika mazingira hayo sekta binafsi ndiyo inachukua nafasi ya kuwa mwajiri mkubwa badala ya sekta ya umma. Katika kipindi hiki Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha kuwa vyama hivi vinaimarishwa na kuwa na sauti ya kutosha ya kutetea maslahi ya wanachama wao na kuhakikisha kuwa Serikali inatunga sheria za kazi

ambazo zitaendelea kulinda na kutetea maslahi ya wafanyakazi katika mfumo wa uchumi wa soko au sekta binafsi.

Vyama vya Ushirika

125**.** Vyama vya ushirika vina sura mbili. Kwa upande mmoja vyama hivyo ni vyombo wanavyotumia wanachama wake kwa ajili ya maendeleo yao ya kiuchumi. Kwa upande wa pili vyama hivyo ni vyombo ambavyo huwapa fursa wanachama wake kushiriki moja kwa moja au kwa njia ya uwakilishi kuviendesha vyama hivyo na kutoa maamuzi mbalimbali kwa manufaa yao ya kimaendeleo. Kutokana na sura hii ya pili ambapo wanachama wanakuwa karibu na vyama katika kuviendesha ndiyo maana vinakuwa ni vyombo muhimu vya upanuzi wa demokrasia ndani ya umma.

126. Kwa kutambua umuhimu wa vyama vya ushirika kama vyombo muhimu vya kidemokrasia katika umma, Chama Cha Mapinduzi kuanzia 2010-2020 kitaendeleza kazi iliyokwishaanza katika miaka iliyopita ya kuhakikisha kuwa Serikali inasimamia kwa dhati utekelezaji wa sera ya maendeleo ya ushirika. Elimu ya ushirika iliyokwishaanza kutolewa katika kipindi kilichopita itaimarishwa ili kuendelea kuwawezesha wanachama wa ushirika kuelewa vizuri dhana ya misingi, kanuni na taratibu za ushirika.

SURA YA SABA

Hifadhi ya Mazingira

"Umaskini na uharibifu wa mazingira ni watoto pacha na mama yao ni ujinga."

A.H. Mwinyi,
Mwenyekiti wa CCM Mstaafu.

127. Umuhimu wa suala la hifadhi ya mazingira kimsingi unaendana na siasa ya CCM ya kupambana na umaskini. Moja kati ya malengo na madhumuni ya CCM ni ***"Kuona kwamba matumizi ya utajiri wa taifa yanatilia***

mkazo maendeleo ya wananchi na hasa jitihada za kuondoa Umaskini, Ujinga na Maradhi" (Katiba ya CCM, ibara ya 5 (14).

128. Mazingira ni nyenzo muhimu ya maendeleo na suala mtambuka, ambalo linagusa sekta mbali mbali za kiuchumi na kijamii. Aidha, upo uhusiano tegemezi kati ya mazingira na maendeleo na kwamba, uharibifu wa mazingira sio tu husababisha umaskini bali umaskini nao husababisha uharibifu wa mazingira.

129. Utafiti juu ya athari za mazingira duniani umebaini kwamba, ingawa uchafuzi wa mazingira umeleta athari mbaya kwa maisha ya binadamu, hata hivyo binadamu mwenyewe mara nyingi ndio chanzo kikuu cha uharibifu wa mazingira hayo.

130. Maendeleo makubwa ya viwanda na matumizi ya sayansi na teknolojia ya kisasa, hususan kwa Mataifa ya Magharibi na Asia, yamesababisha uchafuzi mkubwa wa anga hewa na tabaka la Ozon, pamoja na kuongezeka sana kwa kiwango cha gesi joto angani na kuzuka kwa mabadiliko ya tabia nchi. Kutokana na hali hii, suala la **"Mazingira na Maendeleo"** sasa limekuwa ni ajenda muhimu iliyotanda na kutawala mijadala ya kitaifa na kimataifa, hasa ikizingatia kwamba, matatizo ya uharibifu wa mazingira hayatambui wala kujali mipaka ya nchi.

131. Uchambuzi wa kitaifa juu ya athari za mazingira umebaini kwamba, matumizi ya zana duni katika Kilimo, uvuvi haramu, ukataji wa misitu na uchomaji moto ovyo, ufugaji usiozingatia uwiano kati ya idadi ya mifugo na ardhi, shughuli za uchimbaji wa madini, ujenzi wa viwanda na ongezeko la idadi ya wakaazi katika miji lisiloendana na uwezo wa miundombinu iliyopo, ni miongoni mwa mambo yanaosababisha uharibifu mkubwa wa ardhi, uhaba wa maji safi na salama, ukame na jangwa, upotevu wa viumbe pori na bionuwai**,** uharibifu wa viumbe vya majini na uharibifu wa misitu na milima ya asili.

132. Ili kuondokana na matatizo hayo na kuimarisha udhibiti wa hifadhi ya mazingira katika nchi yetu, CCM itaendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa, Serikali zinaendelea kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake ya kitaifa na kimataifa kwa kuhakikisha upatikanaji na matumizi sawa ya rasilimali kwa ajili ya mahitaji muhimu ya vizazi vya sasa na vijavyo bila ya kuharibu mazingira au kuhatarisha afya na usalama wa binadamu, kuzuia na kudhibiti uharibifu wa ardhi, maji, mimea na hewa ambavyo ndivyo vinashikilia mifumo ya maisha na kuhifadhi na kuimarisha urithi wetu wa asili na usio wa asili, ikiwa ni pamoja na **bioanuwai** zilizo katika mfumo wa kiikolojia wa kipekee wa Tanzania.

133. Vile vile kuboresha hali ya mazingira yaliyoharibiwa ikiwa ni pamoja na makazi ya vijiji na mijini ili Watanzania wote waishi katika mazingira safi na salama, kuongeza utambuzi na ufahamu wa uhusiano kati ya mazingira na maendeleo, na kuendeleza ushirikishwaji wa wananchi na jumuiya zao katika masuala ya hifadhi na utunzaji wa mazingira na kukuza ushirikiano wa kimataifa katika ajenda ya mazingira na kupanua ushirikishwaji na kutoa mchango unaohitajika kwa mashirika na programu za kikanda na kimataifa, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Mikataba ya hifadhi na mazingira duniani.

134. Aidha, kwa kupitia Serikali zake, CCM itahakikisha kuwa, suala la mazingira linasimamiwa vizuri na kupewa umuhimu mkubwa katika kupanga na kutekeleza sera na mipango mbali mbali ya maendeleo na kwamba, suala la kutunza na kulinda mazingira na maliasili zake, linasimamiwa kwa namna ambayo itakuza uchumi wa wanchi na kuleta maendeleo endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

SURA YA NANE

UTAMADUNI NA MICHEZO

Utamaduni

135. Hivi sasa nchi yetu imo katika kujenga utamaduni imara ambao utakabiliana na misukosuko itokanayo na uchumi huria na kunufaika na matunda ya maendeleo ya sayansi na teknolojia. Chama Cha Mapinduzi kitaendeleza harakati za kuenzi na kulinda mila, desturi na maadili mema na kuzitokomeza mila na desturi mbaya. Elimu ndiyo itakayowawezesha Watanzania kuyatambua mazuri ya tamaduni nyinginezo duniani na kuyatumia kuinua ubora wa maisha yao, na wakati huo huo kujikinga na athari za tamaduni za nje zinazodhalilisha utamaduni na utu wa Mtanzania.

136. Fani ya sanaa ni moja ya nyenzo kubwa zilizotumiwa katika harakati za kudai uhuru wa nchi yetu na katika kuongeza kasi ya maendeleo ya jamii. Chama Cha Mapinduzi kitahimiza matumizi ya sanaa katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo na uhuru wetu. Aidha, Chama kitahimiza matumizi ya sanaa katika kampeni za kupambana na matatizo makubwa ya kitaifa kama vile umaskini, ujinga, UKIMWI na kuleta ulingano wa jinsia. CCM itazitaka Serikali zake kuelekeza nguvu katika maandalizi mazuri ya uwanja wa sanaa ili uwe ni kioo cha mwenendo mzuri wa maisha na maadili mema ya wananchi na pia chanzo cha kipato kizuri kwa wasanii wenyewe na kuzielekeza Serikali kusimamia asasi zinazosimamia hakimiliki ili wabunifu wafaidike katika kupata mirahaba ya kazi zao.

137. Kwa kuelewa umuhimu wa Utamaduni na Michezo katika uhai wa Jamii, Taifa halina budi kuweka utaratibu mzuri, malengo yaliyo bora na mikakati maalumu ya kuwashirikisha wananchi katika kuiendeleza sekta hii. Aidha, maudhui ya utamaduni msingi wake ni kumbukumbu na hazina ya urithi katika maumbo yanayoonekana. Hivyo, Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha kuwa inautumia urithi huu kwa ajili ya kutoa mchango mkubwa kwa uchumi wa Taifa letu.

138. Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali zake kujenga nyumba/kumbi za maonyesho ya sanaa ili kupanua wigo wa maeneo ya burudani kwa wananchi. Aidha, CCM itazitaka Serikali zake kukuza Utalii wa kiutamaduni sambamba na utalii wa kimaumbile ili kujenga msingi imara wa utalii endelevu. Utamaduni wetu utumike kusimamia utalii wetu.

Michezo

139. Michezo imekuwa ni eneo moja kubwa la kujenga afya, udugu na mashirikiano. Chama cha Mapinduzi kinakubali mantiki hiyo kuwa kushiriki katika michezo kunachangia kwa kiasi kikubwa katika kuleta hali bora ya maisha, maendeleo na kutangaza na kuinua sifa ya nchi kwa mataifa mengine hivyo basi, Chama cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali zake kuendelea kusimamia michezo yote ikiwemo ya jadi kwa lengo la kuendeleza michezo ya ridhaa pamoja na kuendelea kutafuta wataalamu waliobobea ili kujenga misingi ya michezo ya kulipwa na ajira nyingine kwa vijana.

140. CCM inatambua umuhimu wa michezo katika kujenga afya ya miili na akili.

Hivyo itaendelea kutilia mkazo mkubwa suala la kuendeleza michezo yote nchini ikiwa ni pamoja na michezo ya jadi. Katika miaka kumi ijayo Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali zake kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuandaa utaratibu wa kudumu ambao utawezesha kuziwekea alama maalumu kazi zote za sanaa zilizokaguliwa.

(b) Kuwaendeleza wanamichezo hasa vijana kwa kuwapatia nafasi za kushiriki katika mashindano ya kitaifa na kimataifa na ziara za mafunzo nje ya nchi kwa lengo la kuitangaza nchi yetu kwenye medani ya michezo ya Kimataifa.

(c) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya utamaduni, Sera ya Michezo na kutoa mafunzo ya kiufundi na ya kiutawala kwa walimu na viongozi wa michezo.

(d) Kuwaandaa wanamichezo, kuibua na kutambua vipaji vyao tangu wakiwa shule za msingi ikiwa ni pamoja na kujenga shule maalumu za michezo.

(e) Kuendeleza mazingira ya ushirikiano mzuri uliopo baina ya vyombo vinavyohusika na Utamaduni na vyombo vya habari ili kwa pamoja viendelee kulinda na kuhifadhi Maadili mema ya Watanzania.

(f) Kutenga maeneo/viwanja maalumu kwa ajili ya michezo na kuhakikisha kuwa maeneo hayo hayavamiwi kwa ajili ya shughuli nyingine.

(g) Michezo ni muhimu ianzie kwenye shule, vyuo na katika Majeshi yetu yote.

(h) Kuandaa utaratibu wa mashindano ya michezo katika ngazi ya mkoa, wilaya na vijiji.

SURA YA TISA

SIASA YA MAMBO YA NJE NA UHUSIANO WA KIMATAIFA

141. Siasa ya Chama ya Mambo ya Nje haitengani na siasa ya Chama ya ndani ya nchi. Ni mtiririko na kielelezo cha siasa ile ile ya Chama ya kujenga Taifa jipya lenye mahusiano mapya katika uchumi, siasa na jamii na kati na baina ya mataifa duniani. Lakini uchumi wa nchi ndiyo msingi mkuu wa siasa ya nchi ya mambo ya nje. Uchumi dhaifu unasababisha nchi kushindwa kuamua masuala kwa msingi wa kujitegemea na hivyo kusababisha pia kushindwa kutimiza barabara shabaha ya siasa yake ya mambo ya nje. Ili kuwa na siasa ya mambo ya nje yenye nguvu na kujitegemea ni lazima pia kuwa na uchumi wa ndani ulio imara na wenye kujitegemea pia. Na hii ndio sababu katika kipindi hiki Chama kinalo jukumu la kuhakikisha kuwa nguvu na rasilimali za Taifa zinatumika

kujenga uchumi wa Taifa ulio imara na wa kisasa ili kuweza kuwa na siasa ya mambo ya nje iliyo imara.

Aidha, siasa ya CCM ya Mambo ya Nje itaendelea kuzingatia mambo yafuatayo:-

(a) **Ushirikiano na nchi za jirani na kudumisha umoja wa nchi za Afrika ili**:-

(i) Kudumisha amani kati ya nchi za Kiafrika kwa kuheshimu na kutambua mipaka tuliyorithi wakati wa kupata uhuru;

(ii) Kujenga misingi imara ya ushirikiano wa kiuchumi miongoni mwa nchi za Afrika katika biashara, viwanda na mabadilishano ya teknolojia; na

(iii) Kuendeleza mapambano dhidi ya ukoloni mamboleo.

(b) **Ushirikiano na nchi zinazoendelea**:

Siku zote tumekuwa tayari kushirikiana na nchi yo yote yenye nia njema, ndio sababu tangu uhuru wa nchi yetu mojawapo ya msingi mkubwa wa siasa ya mambo ya nje umekuwa ni siasa ya kutokufungamana na upande wo wote.

(c) **Ushirikiano na vyama rafiki**:

Bara la Afrika bado ni bara la watu waliomo katika unyonge wa kunyonywa na kunyanyaswa. Kwa vyama vya kimapinduzi katika nchi za Afrika zinazojitawala bado vingali ni vyama vya ukombozi. Kwa hiyo ni muhimu kuendelea kudumisha mshikamano miongoni mwa vyama hivi.

(d) **Amani ya dunia**:

Suala la amani linahusiana na suala muhimu la maisha ya binadamu. Hivyo linamhusu kila mtu na kila Taifa. Maendeleo katika uchumi, siasa na ustawi wa jamii yanategemea kuwepo kwa amani na usalama wa dunia nzima. Chama kitaendelea kutoa mchango wake katika juhudi za kuleta amani ya dunia na kupinga njama za kuvuruga amani hiyo.

142. Pamoja na siasa ya mambo ya nje ya Chama Cha Mapinduzi kujikita katika misingi tuliyoitaja hapo juu, Chama kinatambua kuwepo kwa maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia pamoja na utandawazi vitu ambavyo vimeifanya dunia ya leo kuwa kama kijiji kimoja. Maendeleo haya makubwa ya sayansi na teknolojia yaliyofikiwa katika karne ya 21 ni dhahiri yameleta changamoto nyingi mpya za maendeleo kwa mataifa makubwa na mataifa madogo katika bara la Afrika na dunia kwa jumla.

143. Kwa hiyo ili kuendelea kukabiliana na hali hiyo Mwelekeo wa Sera ya CCM ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa katika kipindi cha miaka kumi ijayo (2010-2020) italenga katika kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuitekeleza kwa juhudi na ufanisi Diplomasia ya Uchumi, ili kuiletea nchi yetu maslahi makubwa ya kiuchumi, maendeleo na kuiwezesha kujitegemea.

(b) Kuendeleza Sera ya Ujirani Mwema na Nchi jirani.

(c) Kuimarisha ushirikiano wa kikanda (EAC, SADC, AU,NAM) kwa nia ya kukuza uchumi na maendeleo ya jamii na kujifunza taaluma na mwenendo wa sera za masoko ya biashara za kimataifa, ili kuliwezesha taifa letu kuingia katika soko la dunia lenye ushindani kwa kuzingatia fursa sawa kwa Mataifa yote kibiashara.

(d) Kuendelea kudai mageuzi ya Umoja wa Mataifa, hususan katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kwa lengo la kuongeza sauti na heshima ya nchi zinazoendelea, pamoja na kuendelea kuzishinikiza nchi tajiri kutekeleza ahadi yao ya kutenga asilimia 0.7 ya Pato la Taifa la nchi zao kwa ajili ya misaada kwa nchi maskini.

(e) Kuona kwamba nchi yetu inakuwa karibu na Watanzania wanaoishi ughaibuni ili wachangie katika maendeleo ya nchi yao.

SURA YA KUMI

ULINZI NA USALAMA

"Msingi wa maendeleo ya Ulinzi na Usalama wa Tanzania ni Watanzania wenyewe, kila Mtanzania, na hasa kila mzalendo na kila mjamaa".

Mwongozo wa TANU 1971.

144. Dhana ya Ulinzi wa Umma bado itaendelea kuwa ndiyo Sera ya CCM ya Ulinzi na Usalama katika miaka ya 2010 hadi 2020. Usahihi wa falsafa ya ulinzi wa umma umeendelea kujidhihirisha hata katika kipindi cha miaka kumi iliyopita (2000-2010), ambapo vyombo vya Ulinzi na Usalama vimeendelea kutekeleza majukumu yake ya kufundisha wananchi ulinzi wa umma na kulinda mipaka ya nchi pamoja na kudumisha amani na usalama wa raia na mali zao.

Aidha, vyombo vya ulinzi na usalama vimeshiriki kulinda amani katika maeneo mengine ya Afrika na dunia kwa ujumla.

145. Kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika kipindi hiki Sera za CCM za Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha miaka 2010 hadi 2020, zitaendelea kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendeleza ulinzi wa umma, ambao unawashirikisha wananchi wote ili kuhakikisha kuwa, uhuru wetu na mipaka yetu inadhibitiwa na kuhifadhiwa.

(b) Kuendeleza dhana ya kuwa na jeshi dogo la Ulinzi lenye Viongozi weledi, vifaa, zana na uwezo wa kukabiliana na tishio lolote litakalojitokeza, na lenye mahitaji na matumizi yanayoendana na uchumi wa nchi na mazingira nadhifu ya kufanyia kazi na makazi ambalo litawashirikisha wananchi kama Jeshi la Akiba lililoandaliwa ipasavyo kimafunzo katika jukumu la Ulinzi Jamii.

(c) Kuimarisha uwezo wa vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama vikiwemo Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto pamoja na Vikosi vya SMZ kwa mafunzo, vifaa na zana za kisasa, ili kuviongezea uwezo na mbinu za kuweza kudhibiti vitendo vya ujambazi, machafuko katika jamii, madawa ya kulevya, uhamiaji haramu, kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo na aina nyingine za uhalifu pamoja na kukabiliana na maafa na majanga mbalimbali.

(d) Kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ambavyo ni vyuo vya kuwajenga vijana wa Kitanzania katika uzalendo, ukakamavu, usawa na umoja wa Kitaifa, na kuwaandaa katika uzalishaji mali na stadi mbali mbali za ufundi; na kuwa ndio chimbuko la ajira kwa vyombo vya Ulinzi na Usalama hapa nchini pamoja na shughuli zote za kiuchumi na uzalishaji mali.

(e) Kuendelea kuliimarisha Jeshi la Magereza ili liwe chombo cha uzalishaji wa kisasa katika kilimo na ufugaji.

(f) Kuwa na vituo vya Utafiti na Uendelezaji wa teknolojia ya kisasa pamoja na viwanda vya kijeshi vyenye uwezo wa kuzalisha bidhaa zinazokidhi mahitaji halisi ya matumizi ya kijeshi na kiraia.

(g) Kuunga mkono jitihada za Umoja wa Nchi huru za Afrika (AU), Umoja wa Mataifa (UN) na Jumuiya za Kikanda na kushiriki kikamilifu katika kusimamia utatuzi wa migogoro na ulinzi wa amani (Peace keeping), ndani ya Bara letu la Afrika na Dunia kwa jumla.

146. Kuhusu suala la kurejesha mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria kwa vijana wanaomaliza elimu ya juu Chama Cha Mapinduzi kinasisitiza mambo yafuatayo yazingatiwe:-

(a) Yafanyike maandalizi ya kutosha kwa kuzingatia mabadiliko

yaliyotokea katika kipindi ambacho JKT ilikuwa imesimamisha mafunzo yake;

(b) Izingatiwe kuwa idadi ya walengwa sasa ni kubwa kuliko hapo awali;

(c) JKT liwe na uwezo wa kujitegemea;

(d) JKT kiwe ni chombo thabiti cha kujenga maadili ya umoja wa kitaifa, uzalendo na maadili ya kupenda kazi miongoni mwa vijana watakaopitia katika jeshi hili; na

(e) Katika maandalizi ya sasa ya kurejesha mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria, yafanywe maandalizi ya kutosha.

SURA YA KUMI NA MOJA

CHAMA CHA MAPINDUZI NA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA MWELEKEO 2010-2020

"Chama imara ni kile ambacho viungo vyake vimekamilika na vinafanya kazi vizuri. Chama ni wanachama, viongozi, vikao, watendaji, rasilimali na Jumuiya za Chama".

Jakaya Mrisho Kikwete
Mwenyekiti wa CCM.

147. Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2010 hadi 2020 unaainisha majukumu makuu yaliyo mbele yetu kuwa ni:-

(a) Kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea na

(b) Kutekeleza sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

148. Makusudio ya Chama ni kuwa majukumu hayo makuu yakitekelezwa ifikapo mwaka 2020 nchi yetu itakuwa inakaribia kufikia lengo letu la kuwa nchi yenye maendeleo ya wastani. Maana yake ni kuwa vita dhidi ya maadui wetu wakubwa ujinga, umaskini na maradhi itakuwa imezaa matunda kwani ujinga na umaskini utakuwa umefutwa kwa sehemu kubwa na maradhi yatakuwa yamedhibitiwa. Hali hii italeta ukombozi kwa wananchi walio wengi.

149. Katika mambo makubwa yanayoainishwa kisera katika Mwelekeo na kutafsiriwa katika Ilani za miaka mitano mitano kwa utekelezaji, sehemu kubwa ni mambo yanayotekelezwa na Serikali lakini machache yanayobaki yanatekelezeka kupitia Chama na wananchi wenyewe. Yale yanayohusu Serikali yatatekelezwa kwa mujibu wa mifumo na taratibu za kiserikali. Hapa si mahali pake pa kuyachambua. Yamezunguzwa katika Utangulizi wa Mwelekeo huu. Hapa tuzungumzie yale mambo yanayohusu Chama chenyewe.

Wajibu wa CCM katika kufanikisha Utekelezaji na Mwelekeo na Ilani zake

150. Chama kione kwamba uongozi wa Chama na wanachama wanakuwa na uelewa unaofanana wa Sera, mikakati na majukumu yaliyoainishwa katika Mwelekeo wa Sera za CCM wa 2010 hadi 2020 na Ilani za Uchaguzi za 2010-2015 na 2015-2020. Lengo hili litafanikiwa kwa Chama kuendesha mafunzo, semina na madarasa ya itikadi kwa viongozi wa ngazi mbalimbali na pia kwa wanachama. Chama kinatakiwa kiandae mpango wa kitaifa wa kutekeleza jukumu hili.

151. Kutokana na kwamba utekelezaji, wa wajibu uliotajwa hapo juu unahitaji usimamizi wa karibu wa viongozi wa kitaifa, mkoa na wilaya, **uwepo mpango maalum wa mafunzo** kwa viongozi wa ngazi hizo mara baada ya Uchaguzi Mkuu kuisha na Serikali mpya kuundwa. Kwa kufanya hivyo Chama kitakuwa na safu ya viongozi wa ngazi hizo wenye uelewa mmoja wa Sera na majukumu makuu ya kutekelezwa katika kipindi cha sasa cha Mwelekeo na Ilani.

Kuhusu kufanikisha Mapinduzi ya Kilimo na Ufugaji

152. Mapinduzi ya Kilimo na ya ufugaji yana mambo makubwa yafuatayo:-

a) Upatikanaji wa Maji.
b) Kanuni za Kilimo/Ufugaji bora (maarifa).
c) Mbegu bora, mbolea na madawa.
d) Zana bora (za kisasa).

153. Kama maji yapo, jambo la msingi la kuingia katika Mapinduzi ya kilimo ni kutekeleza kanuni za kilimo bora ambazo ni pamoja na matumizi ya mbegu bora, mbolea na madawa. Kwa kuzitekeleza kanuni za kilimo bora, tija katika mavuno inaweza kuongezeka mara mbili, tatu hata zaidi katika eneo lile lile la zamani.

Chama na Mapinduzi ya Kilimo

154. Ili kuleta Mapinduzi ya kilimo Chama Cha Mapinduzi kiwe chachu. Kwanza viongozi wa Chama wajifunze kanuni za kilimo bora za mazao wanayoyalima pale walipo. Baada ya kupata mafanikio katika mashamba yao, washirikiane kuwaelimisha wanachama wenzao katika tawi ili nao wazifahamu kanuni za kilimo bora kwa kutumia mafanikio ya mashamba ya viongozi na kuyatumia kama mfano. Hatua ya tatu, Chama katika tawi husika, kitumie mafanikio ya mavuno bora na mengi ya wanaCCM kuwashawishi wanakijiji wote kijijini kufuata mfano wa mafanikio ya mazao bora na mengi kwa wao nao kutekeleza kanuni za kilimo bora. Hii ndiyo maana ya Chama kuwa chachu katika kusukuma maendeleo na mabadiliko vijijini. Chama katika kijiji kikitimiza jukumu lake hili la kuongoza kwa kuonyesha njia, maisha ya wanaCCM na wanavijiji kwa ujumla yatabadilika na kuwa bora maana kilimo chao kitakuwa kina tija kubwa na chenye kuzalisha ziada.

155. Mkakati huu wa Chama kuwa chachu ya kuleta mabadiliko katika jamii kutokana na Chama chenyewe kuonyesha njia kwa kupitia viongozi na wanachama wake utumike pia kuleta Mapinduzi ya ufugaji ili kuliondoa Taifa kutoka ufugaji wa jadi na kuingia kwenye ufugaji bora wa kisasa wenye tija kwa wafugaji.

Chama na Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi

156. CCM ina wajibu mkubwa katika mchakato wa kuitekeleza sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Baadhi ya majukumu ya Chama ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha viongozi na wanachama wa CCM wanaielewa vema sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, chimbuko lake, umuhimu wake na mikakati yake.

(b) Kuwatanabaisha viongozi, wanachama na wananchi kuwa uwezeshaji wa kwanza unamhusu mwananchi mwenyewe, kila mwananchi, kuendeleza vipaji alivyonavyo na kujituma kwa kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili ajiletee maendeleo yake na familia yake. Ni watu wenye kujituma tu ndio wanaoweza kufaidika na fursa zilizopo nchini za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

(c) Ofisi za CCM nchini zitumike kutoa ushauri kwa viongozi, wanachama na wananchi kuhusu fursa zilizopo za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Jumuiya za CCM pia zinaweza kujipanga kutekeleza wajibu huu.

Chama Cha Mapinduzi na Ushirika

157. Kwa mujibu wa Itikadi ya CCM ya Ujamaa na Kujitegemea, Ushirika huru wa wananchi ni muhimu kwa itikadi hiyo. Ushirika wa aina mbalimbali ukiundwa na kuendeshwa kwa misingi na kanuni sahihi, ni njia muafaka inayowawezesha wananchi, hasa wa kawaida, kumiliki na kuendesha uchumi katika nchi yao. Aidha, ushirika umesimama kwenye msingi kwamba umoja ni nguvu.

158. Aidha, ushirika ni chombo muhimu kinachoweza kuwaunganisha wanyonge katika jamii wapate nguvu ya kutetea na kuendeleza maslahi yao dhidi ya nguvu za unyonyaji na ukandamizaji na dhuluma. Vile vile ushirika, hasa ushirika wa mazao, wafugaji na wavuvi, ushirika wa viwanda vidogo vidogo, ushirika wa wachimba madini wadogo wadogo na ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS), unatoa mchango mkubwa katika ujenzi wa nchi yetu.

159. Kwa kuzingatia umuhimu wa ushirika kama chombo cha ukombozi wa wanyonge katika kujiletea maendeleo yao, CCM ina wajibu wa kuipandisha juu bendera ya ushirika kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kuanza upya vuguvugu la kichama la kueneza elimu na kusisitiza juu ya umuhimu wa ushirika kwa maendeleo ya wananchi.

(b) CCM iwahimize wanachama wake na viongozi kujiunga na ushirika pale walipo katika ushirika wa aina mbali mbali.

(c) CCM ihimize Serikali kuendelea na mipango ya kufufua ushirika hasa kwa kuwaandaa maafisa ushirika wa fani zote muhimu ili vyama vya ushirika vipate ushauri wa kitaalamu unapohitajika.

(d) Hapo juu tumefafanua juu ya Mapinduzi ya kilimo na kukitaka Chama kiwe chachu, katika kufanikisha utekelezaji wa kanuni za

kilimo bora ili kiwe na tija na mavuno yawe mengi katika eneo dogo. Mapinduzi ya kilimo itabidi yafuatiliwe na matumizi ya zana bora ili kumpunguzia mkulima harubu na pia kumwezesha kuwa na shamba kubwa zaidi.

Lakini zana za kisasa ni ghali. Ni vigumu kwa mkulima mmoja kuzimudu gharama zake. Hivyo ushirika ni njia ya uhakika ya kuwawezesha wakulima wanaushirika kumiliki zana bora. CCM kwa kupitia wanachama wake iwe mstari wa mbele kupigania mipango ya ushirika kumiliki zana bora mana zana bora ni sehemu ya ukombozi katika maendeleo ya binadamu.

160. Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka 2010-2020 unatoa wito wa kufanya Mapinduzi ya kiuchumi na kijamii ili mwishoni mwa miaka kumi kuanzia sasa hali ya maisha ya Watanzania iwe bora zaidi kiuchumi na kiustawi wa jamii. Sura hii ya Chama Cha Mapinduzi inasisitiza kuwa ili jambo lifanikiwe lazima liwe na wenyewe. Sera hizi za miaka ya 2010 hadi 2020 ni za CCM. Wenyewe ni viongozi na wanachama, hivyo wajitokeze kuzitekeleza kwa vitendo. Wananchi watafuata mfano wetu na hapo malengo yetu yatafanikiwa.